SportPesa
TZS. 1,119,012,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Watalii** 961 kumiminika nchini wiki hii

UKURASA 4



**VAN GAAL ASUMBULIWA TEZI DUME**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumanne Aprili 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580906

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Wadau wapongeza Bunge 'live' kurejea

• **Wabunge** kupokea ripoti uchafuzi Mto Mara... *Endelea ukurasa 3*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**SITA WAFARIKI KATIKA AJALI MBILI ZA GARI**
WATU sita wamefariki dunia na wengine 25 kujeruhiwa katika ajali mbili tofauti...

UKURASA WA 5
**WACHANGISHWA 10,000/- WASIHAMISHWE NGORONGORO**
BAADHI ya wananchi wanaoishi eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro...

UKURASA WA 5
**NHC KUJENGA NYUMBA ZAIDI DAR NA DODOMA**
SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limetaja vipaumbele 11 vitakavyoanza kutekelezwa...


## CHADEMA, NCCR wasusa kongamano la haki, maridhiano

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akimsikiliza Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo kwenye uzinduzi wa ugawaji wa vitendea kazi kwa maofisa ugani jana, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Samia aridhia maofisa ugani kumilikishwa pikipiki miaka 2

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA MDOMONI MWA VINARA CAF** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo na Utafiti wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Pedro Pallangyo, akiwaelezea huduma zinazotolewa na taasisi hiyo wanafunzi kutoka Shule ya Heaven of Peace Academy ya jijini Dar es Salaam waliotembelea JKCI kwa ajili ya kujifunza magonjwa ya moyo kwa vitendo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia aridhia maofisa ugani kumilikishwa pikipiki miaka 2

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekabidhi pikipiki 70,000 kwa maofisa ugani wote nchini ikiwa ni jitihada za serikali za kuboresha huduma za ugani ili kukuza sekta ya kilimo nchini.

Rais aliyasema hayo jana jijini Dodoma katika hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa vitendea kazi kwa maofisa ugani kilimo.

Rais alikubali ombi la Waziri Kilimo, Hussein Bashe la kuwamilikisha maofisa ugani pikipiki walizopatiwa leo baada ya miaka miwili ziwe mali yao kwa masharti ya kupimwa kwa huduma watakazotoa.

"Nafikiri miaka miwili ni muda mzuri, kwa sababu tukiwaambia miaka miwili maofisa ugani watazitunza pikipiki na akijua miaka miwili ikimalizika itakuwa yake atajtunza," alisema.

Maofisa hao pia wamegawiwa simu janja ili kurahisisha utendaji kazi wao wakiwa katika maeneo ya kazi, huku Rais akiagiza wapatiwe sare ili iwe rahisi kutambulika kama walivyo wafanyakazi wa sekta nyingine.

Akizungumza katika hafla huyo Rais Samia alisema sekta ya kilimo ni muhimu kwa ustawi wa Watanzania na imeendelea kuwa mhimili mkuu na muhimu wa kukuza uchumi wa taifa na kuleta maendeleo. Kwa mwaka 2020 sekta hiyo ilikuwa kwa asilimia 4.9 na kuchangia asilimia 26.9 kwenye pato la taifa.

"Lakini ilitoa ajira kwa asilimia 61 ya Watanzania na kuchangia asilimia 65 kwenye malighafi za viwanda, kwa hiyo kwa takwimu hizo utaona kuwa sekta hii imechangia tujitosheleze kwa chakula kwa asilimia 100," alisema.

Alisema pamoja umuhimu wa sekta hiyo katika taifa bado ukuaji wake ni mdogo, hivyo kunahitajika jitihada kuongezwa ili kuifanya kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania kama Hayati Mwalimu Julius Nyerere alivyoelekeza.

Alisema katika kuweka jitihada hizo ilani ya Chama Cha Mapinduzi iliwekea malengo matano ikiwamo kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo kutoka asilimia 5 hadi 5-7 kama ilani ilivyoelekeza huku malengo yakiwa ni kukua kwa asilimia 10 kufikia 2025.

"Lakini tulisema kuongeza thamani ya mazao tunayoyauza nje kutoka dola bilioni 1.2 hadi dola bilioni 5, lakini kama tukifuata mpango wa pili wa kilimo Tanzania basi tunakwenda kuvuka hapo," alifafanua Rais.

Rais alisema lengo lingine ndani ya ilani hiyo ni kuongeza idadi ya mashamba makubwa kutoka hekta 110 hadi 1000, kuongeza hekta za eneo la umwagiliaji maji kutoka hekta 695,000 hadi mil 1.2 huku lengo la serikali ni kufikia hekta milioni 18.

Alisema katika kuhakikisha kuwa malengo hayo yanatekelezeka kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha 2021-2026, serikali imeongeza bajeti ya utafiti kutoka Sh. bilioni 7.35 hadi 11.

"Haya yote tumeyaongeza kwa sababu, mimi ni muumini mkubwa, kwamba kilimo kitaivusha nchi na nimefanya kazi ya kilimo kwa miaka kadhaa kama 9, upande wa mifugo na upande wa chakula chini ya Shirika la Chakula Duniani...na nimeona ni vitu gani vikifanywa kilimo kinakwenda kupanda vizuri," alisema.

Alisema suala la pili ni kuongeza bajeti ya huduma za ugani kutoka Sh. bilioni 17.7 hadi Sh. bilioni 51.45. Huku fedha za uzalishaji wa mbegu zikiongezwa kutoka Sh. bilioni 5.42 hadi Sh. bilioni 10.58.

Rais aliongeza kuwa wamefanikisha kuongeza soko la mazao ya chakula nje ya nchi hususani parachichi katika nchi za India na Afrika Kusini baada ya kukidhi ubora, pamoja na kughala ya chakula nje ya nchi.

"Tunafanya jitihada zote hizi ili wakulima wapate thamani ya jasho wanalolilotoa, wale watu wa katikati wa kwenda kununua mazao kwa bei ya chini yeye akaenda kuuza kwa bei ya juu hapana," alisisitiza Rais.

Aliagiza kuwapo na mfuko wa mzunguko wa pembejeo na maendeleo ya kilimo ili ikasaidie pale bei za pembejeo zitakapopanda pamoja na kusaidia jumuiya za umwagiliaji.

Alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, awashughulikie walioiba fedha za pembejeo za ruzuku na za ushirika ili iwe fundisho kwa wengine.

Kadhalika, aliagiza mashamba yaliyokuwa chini ya Msajili wa Hazina yatumike katika uzalishaji badala kukaa bila ya shughuli yoyote kama yaliyo sasa.

Naye Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema kuwa kupitia ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 na ya 2025 iliweka mkazo katika serikali yake kusimamia kilimo kuanzia maandalizi mpaka masoko.

Akirejea kauli ya Rais Samia wakati akiwa Makamu wa Rais ya kuwa ili nchi iweze kupata mafanikio ya kiuchumi ni lazima ijikite katika kilimo, kwa kuwa asilimia 60 ya Watanzania wanajishughulisha na kilimo.

Alisema ndipo serikali ikaanza kuwekeza kwenye mazao matano ya kimkakati yanayolimwa na watu wengi ikiwamo korosho, chai, pamba, kawana na tumbaku na sasa wamepanua wigo kwa kuongeza mazao ya mafuta ikiwamo mchikichi na alizeti ili kujipunguzia mzigo wa kutumia zaidi Sh. bil. 470 kila mwaka kuingiza mafuta.

KUMBUKUMBU MIAKA 100 YA NYERERE

## Wanasiasa waaswa sio kutafuta mali, umaarufu

**Na Romana Mallya**

WANASIASA hasa vijana wametakiwa wasifanye siasa kama ni kinyang'anyiro cha kutafuta madaraka, mali na umaarufu kwa sababu hata Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere pamoja na ushawishi aliokuwa nao aliingia kwa lengo la kuipigania nchi.

Hayo yalisemwa jana mkoani Dar es Salaam na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, katika kongamano la miaka 100 la kuzaliwa kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere (MNMA).

Kongamano hilo lilibebwa na mada: "Misingi na urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kujenga amani, umoja na maendeleo ndani na nje ya Afrika."

Akifungua kongamano hilo, Prof. Mkenda alisema, Mwalimu Nyerere aliingia kwenye siasa kwa hamasa ya dhati ya kupigania nchi na sio kwa umaarufu wala mali.

"Aling'atuka mwenyewe hakulazimishwa, angeweza kubadilika, lakini alisema aingie mwingine aendelee. Tuliopo kwenye siasa kwa sasa hasa vijana msiingie kwa kufanya siasa ni kinyang'anyiro cha kutafuta madaraka, mali na umaarufu.

"Tuingie kwa moyo wa uanaharakati wa kujaribu kuleta maendeleo ya nchi. Mwanasiasa kazi yake kubwa ni kushawishi, Mwalimu Nyerere alitembea na Land Rover nchi nzima barabara zikiwa vumbi akipandisha kioo joto, akishusha kioo vumbi alizunguka nchi nzima kwa miaka saba kushawishi watu tupate uhuru, kazi ya siasa haibadiliki lazima iwe na mwelekeo wa kujitolea kwa namna moja."

Prof. Mkenda alisema wanamkumbuka Mwalimu Nyerere kwa sababu alikuwa mwenye maono na falsafa aliyoieleza na kuitekeleza, aliamini binadamu wote ni sawa na dhana ya usawa wa binadamu kwake ilikuwa ni ya muda mrefu.

Alisema aliongoza taifa bila ubaguzi na alijenga nchi kutoka viwango vya chini vya kiuchumi.

Mwenyekiti wa bodi ya chuo hicho, Stephen Wassira, alisema Mwalimu aliamini katika usawa wa kibinadamu, umoja na aliondoa ubaguzi wa dini, kabila na rangi.

"Alipenda amani, uhuru wa Afrika, alishirikiana na wapigania uhuru wa Afrika," alisisitiza.

Aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), Ludovick Utouh, katika mada yake iliyomzungumzia Mwalimu Nyerere na diplomasia ya kimataifa, alisema alikuwa na uwezo mkubwa na nguvu ya ushawishi na mwenye maono.

Alisema alitambua umuhimu wa uhusiano na nchi nyingine duniani na Tanzania ilishiriki kikamilifu katika mambo yanayohusu diplomasia ya dunia.

Alisema alikuwa muumini wa uwapo wa maelewano na mshikamano na nchi za Afrika.

Pia alisema Mwalimu Nyerere ndiye Rais wa kwanza Afrika kujiuzulu kwa hiari yake mwenyewe na aliyetembelea nchi nyingi zaidi baada ya kustaafu kuliko alivyokuwa madarakani.

Mhadhiri MNMA, Dk. Bertha Losioki, katika mada yake iliyomzungumzia Mwalimu Nyerere katika amani na mshikamano Afrika, alisema mara zote alisisitiza amani katika kujenga Uhuru wa Tanganyika na umoja miongoni mwa wanawake na wanaume.Alisema aliamini umoja wa kitaifa na baada ya uhuru baraza lake la mawaziri lilijumuisha watu kutoka maeneo tofauti kwa kuhakikisha kunakuwa na fursa sawa.

Alisema alitumia lugha ya Kiswahili ambayo iliwaleta watu pamoja na kusaidia kufanikisha upatikanaji wa uhuru.

"Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliimarisha umoja, unaendelea kuwaleta Watanzania pamoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali, muungano ni mshikamano nzuri wa umoja na amani. Mwenge unaopita mikoa mbimbali unaendelea kujenga mshikamano na uchumi wa nchi," alisema.

Alisema Nyerere alichangia kwa kiasi kikubwa kujenga uhuru na mshikamano barani Afrika.

Waziri mstaafu, Prof. Palamagamba Kabudi katika mada yake Mwalimu Nyerere katika kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi alisema alikuwa na dhana ya kujenga taifa lenye makabila 120 na ujenzi wa taifa unaozungumzia maendeleo ya kijamii na uchumi wa Tanzania.

Awali, Mkuu wa chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema MNMA ni kitovu cha utoaji wa elimu, mafunzo na maarifa na kuendeleza amani na umoja wa taifa.

HABARI KITAIFA

# Wadau wapongeza kurudi Bunge 'live'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE mubashara litaanza kurushwa rasmi katika vikao vyake vinavyoanza leo baada ya kusitishwa kwa miaka sita

Hatua hiyo imepongezwa na wadau mbalimbali kuwa itaongeza uwazi na uwajibikaji wa wabunge kwa wananchi.

Katibu wa Bunge, Mnenelwa Mwihambi, alitoa taarifa hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano wa saba wa Bunge la 12, unaoanza vikao vyake leo jijini Dodoma.

Mwihambi alisema hatua hiyo ya kurusha matangazo ya Bunge moja kwa moja imetokana na Kamati ya Uongozi ya Bunge kuridhia.

"Mnafahamu kuna studio ya Bunge ambayo tumeanzisha mwaka 2016 na tangu ianzishwe tumekuwa tukifanyia maboresho kwa maana ya wataalamu, vifaa na miundombinu, sasa nimewaita niwajulishe rasmi maboresho yamekamilika."

"Kamati ya uongozi leo imeridhia kuanzia sasa tutaendelea kurusha matangazo ya Bunge 'live' kwa maana ya kwamba vituo vya redio, runinga na mitandao ya kijamii itakayotaka kurusha matangazo itachukua kwenye studio yetu moja kwa moja na wenyewe watarusha moja kwa moja," alisema.

**RIPOTI MTO MARA**

Katika hatua nyingine, ripoti ya kitaalamu ya uchafuzi wa Mto Mara leo itawasilishwa kwa wabunge.

Alibainisha kuwa katika kikao cha leo shughuli zitakazofanyika ni kiapo cha uaminifu kwa Mbunge wa kuteuliwa, Shamsi Vuai Nahodha, ambaye anajaza nafasi iliyoachwa na Humphrey Polepole ambaye ameteuliwa kuwa Balozi nchini Malawi.

"Tutaanza na kiapo, halafu maswali na baada ya hapo wabunge watatoka na kuja Msekwa (ukumbi) kwa ajili ya kikao kazi au semina na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ili kupokea taarifa ya kitaalamu ya uchunguzi uliofanywa kutokana na uchafuzi wa Mto Mara," alisema.

Alisema kuwa shughuli za bajeti zitaanza kesho na bajeti kuu ya serikali itasomwa Juni 16, mwaka huu.

MAONI YA WADAU

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Paul Loisulie, amesema kurushwa kwa Bunge mubashara wananchi watapata fursa ya kufuatilia kinachoendelea kuhusu nchi yao.

"Suala la uwazi katika uendeshaji wa derikali ni la kidunia, wenzetu Wakenya wameshafika mbali sana maana usikilizaji wa kesi kubwa kubwa unarushwa mubashara, usaili wa nafasi za juu za uteuzi serikali unarushwa mubashara. Hivyo sisi Tanzania tulikosea sana sana kuondoa Bunge mubashara. Nawapongeza wahusika kwa kurudisha, rai yangu tusirudi nyuma tena," alisema.

Alisema Bunge mubashara lilisitishwa wakati wa serikali ya awamu ya tano na limerejeshwa na serikali ya awamu ya sita.

"Jambo la kwanza na la muhimu ni kwamba kauli ya Mzee Mwinyi ya kila zama na kitabu chake imedhihirika, awamu ya tano ilikataa kurushwa vikao vya Bunge mubashara, awamu ya sita imerejesha, sababu ya Bunge mubashara kurudishwa ni jitihada za Rais Mama Samia kujisimika na kujipambanua kuhusu masuala ya uwazi, ushirikishwaji, utawala wa sheria na misingi ya utawala bora kwa ujumla," alisema.

Mkurugenzi wa MISA-Tanzania, Fumbuka Ng'wanakilala, alisema uamuzi wa Bunge kurejesha matangazo ya vikao vya Bunge yaonekane mubashara ni utekelezaji wa matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kila Mtanzania ana haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa kuhusu masuala mbalimbali kwenye jamii inayomzunguka, haki hii inalindwa na kusimamiwa chini ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Alitoa wito kwa mamlaka mbalimbali nchini kutekeleza na kuheshimu matakwa ya Katiba, sheria za nchi na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania imesaini na kuridhia inayotoa uhuru wa habari, uhuru wa kutoa mawazo na haki ya raia kupata taarifa

"Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema "Tunapongeza sana kwa hatua hii ilikuwa imechelewa maana wananchi walikuwa hawajui wawakilishi wao wanajadili nini."

Alisema kurudishwa kwa mijadala 'live' kutaweka uwajibikaji zaidi kwa wabunge na waajiri zaidi kwa wapiga kura.

# Sita wafariki katika ajali mbili za gari

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,** DODOMA

WATU sita wamefariki dunia na wengine 25 kujeruhiwa katika ajali mbili tofauti zilizotokea eneo la Chamwino na Mpwapwa mkoani Dodoma.

Katika ajali iliyotokea Chamwino, watu wanne wamepoteza maisha na wengine 19 kujeruhiwa baada ya basi la Kampuni ya Geita Express, lenye namba za usajili T 640 DLE linalofanya safari za Dar es Salaam kwenda Geita, kugongana na gari la mizigo lenye namba za usajili T 134 DXR aina ya Fuso katika Kijiji cha Manchali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, akizungumzia ajali hiyo juzi katika eneo la tukio, alisema chanzo ni uzembe wa dereva wa gari ya mizigo aliyejaribu kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari.

Kamanda Lyanga alisema, majeruhi wa ajali hiyo walifikishwa katika Hospitali ya Uhuru, Wilaya ya Chamwino na kupatiwa matibabu.

Alisema kati ya vifo hivyo mmoja ni mwanamume na aliyetambulika ni Sila Elias (19) mkazi wa Mbande, mkoani Dodoma aliyekuwa anajishughulisha na biashara ndogo za kuuza maji katika mabasi.

Katika ajali nyingine iliyotokea Aprili 2, majira ya saa 2:30 asubuhi njia panda ya Mpwapwa, Wilaya na Kongwa basi lenye namba za usajili T.144 DLK aina ya Eicher lililokuwa likitokea Kijiji cha Mkoka kwenda Mpwapwa, lilianguka na kusababisha vifo vya watu wawili na majeruhi sita.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together, we can build a better life)

## PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019.

| | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | | | |
| a) Monthly | | FREE | | FREE |
| b) Interm | | TZS 4,300.00 | | $ 5.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | | FREE | Up to 5000 | FREE |
| | | | Above 5000 | 0.26% |
| 5. Cash Deposit Charges | | FREE | | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | | TZS 12,800.00 | | $ 6.00 |
| 7. A/c Closure charges | | TZS 12,800.00 | | $ 13.00 |
| 8. Activation of Dormat A/c | | TZS 5,100.00 | | $ 6.00 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly | | TZS 4,300.00 | | $ 5.00 |
| b) Interm | Fixed | TZS 4,300.00 | Fixed | $5.00 |
| | plus For each page | TZS 500.00 | For each page | $1.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MILLION | FREE | Upto 5000 | FREE |
| | ABOVE 25 MILLION | 0.11% | 5000 to 10,000 - | 0.26% |
| | | | Above 10,000 | 0.43% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO | FREE | Upto 10,000 | FREE |
| | ABOVE 50 Million | 0.11% | > 10,000- | 0.26% |
| 5. Balance Confirmation certificate | | TZS 21,200.00 | | $13.00 |
| 6. Stop Payment Charges | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| 7. Cheque Clearing Charges | | | | |
| a) Inward | | TZS 1,300.00 | | $1.00 |
| b) Outward | | FREE | | FREE |
| 8. Cheque Return Charges | | | | |
| a) Inward | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| b) Outward | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| 9. A/c closure charges | | TZS 21,200.00 | | $17.00 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | | | |
| **1. Cash Withdrawal** | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS 1,700.00 | | NA |
| 101,000 to 200,000 | | TZS 2,600.00 | | NA |
| 201,000 to 400,000 | | TZS 4,300.00 | | NA |
| 401,000 to 600,000 | | TZS 5,100.00 | | NA |
| 601,000 to 999,000 | | TZS 6,800.00 | | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS 500.00 | | NA |
| 101,000 to 250,000 | | TZS 900.00 | | NA |
| 251,000 to 500,000 | | TZS 1,700.00 | | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | | TZS 4,300.00 | | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | | TZS 8,500.00 | | NA |
| **Mobile Banking Services** | | | | |
| A) Monthly Subscription Charges | | TZS 500.00 | | NA |
| B) PIN Request | | TZS 2,200.00 | | NA |
| **D. LOCKERS RENT YEARLY** | | | | |
| 1.SMALL | | TZS 296,700.00 | | NA |
| 2. MEDIUM | | TZS 508,500.00 | | NA |
| 3. BIG | | TZS 635,600.00 | | NA |

| E. REMITTANCES | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| 1. TISS | TZS | 8,450.00 | EQUIVALLENT TO TZS 8450 | |
| **2. E Remittances** | | | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | TZS | 17,000.00 | $ | 9.00 |
| 1001 to 5000 | TZS | 20,400.00 | $ | 11.00 |
| 5001 to 10000 | TZS | 40,700.00 | $ | 22.00 |
| 10,001 and above | TZS | 84,800.00 | $ | 43.00 |
| **3. SWIFT** | | | | |
| **a) Swift Outward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 39.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 51.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 77.00 |
| **b) Swift Inward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 11.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 16.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 26.00 |
| **F. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 5,000 - | $85.00 |
| | 5Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 5000 to 10,000 - | $170.00 |
| | 10 Mio to 25mio - TZS | 339,000.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | 20,000 to 500,000 - | 1.28% |
| | >500mio--* (*minimum 7,5mio) | 1.06% | >500,000--* (*minimum 7,500) | 1.06% |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | Upto 50,000 FREE | |
| | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | >50,000 - (Min 150) | 0.26% |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 5 Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 20,000 to 500,000 - | 1.53% |
| | 10Mio 25mio - TZS | 381,400.00 | >500,000--* (*minimum 9000) | 1.28% |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | | |
| | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | | |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 50,000 | $22.00 |
| | >100 mio - TZS | 42,400.00 | >50,000 | $43.00 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS TZS | 101,700.00 | | $43.00 |
| 6.Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 1.70% | of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 1.70% |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | | | |
| Bonds & Guarantees | ( Min TZS 75,000) | 1.02% | | 1.02% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | | 0.43% |
| **H. LETTER OF CREDIT** | | | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | | |
| Opening commission | | NA | ( Min $ 200) | |
| LC amendment Commission | | NA | ( Min $50 max 350) | 1.02% |
| Swift charge for LC opening | | NA | | 0.34% |
| Swift charge for other message/amendments | | NA | | $34.00 |
| Extensions - Commissions | | NA | ( Min $200) | $34.00 |
| LC cancellation charges | | NA | ( Min $200) | 1.02% |
| Non payment of Bills on due date | | NA | Till Payment | 1.02% |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | | |
| Advising commission | | NA | | $119.00 |
| Confirmation Commission | | NA | ( Min $150) | 0.43% |
| Negotiating bills under LC | | NA | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Reimbursement claim paid | | NA | ( Min$75) | 0.43% |
| Extensions - Commissions | | NA | ( Min $200) | 1.02% |
| Collection of Export LC | | NA | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Amendments | | NA | | $64.00 |

### OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |

i. Fixed Deposits of TZS

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

ii. Fixed Deposits of USD

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 01-04-2022 |
| SALMA MRISHO | HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | SIGNED | 01-04-2022 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 01-04-2022 |



Waziri wa Maliasili na Utalii Balozi, Dk. Pindi Chana (kulia) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), George Simbachawene, wakiweka saini nyaraka za makabidhiano ya ofisi ya Waziri Mkuu juzi jijini Dodoma. Kushoto ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Ummy Ndalienanga. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# CHADEMA, NCCR wasusa kongamano haki, maridhiano

**Na Maulid Mmbaga**

VYAMA vya CHADEMA na NCCR-Mageuzi, vimesema havitashiriki kongamano la haki na maridhiano lililoandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), kwa madai ya kutokuwa na imani na mwenendo wa kituo na kutojua kinachoenda kuridhiwa.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa TCD, Zitto Kabwe, alipoulizwa kama vyama vyote vilishirikishwa katika maandalizi na kama vimethibitisha kushiriki, alisema msimamo wa CHADEMA ni wa siku nyingi kuwa hawatashiriki, lakini NCCR siyo wa kweli.

"Sio ya kweli, NCCR walishiriki vikao vyote vya maandalizi ya mkutano, kikao cha mwisho cha viongozi wakuu wa vyama kilichofanyika Machi 11, mwaka huu kiliwakilishwa na viongozi wao wa kitaifa," alisema na kuongeza:

"Kamati ya maandalizi ina wajumbe kutoka NCCR-Mageuzi, pia wana sababu tofauti sio hizi wanazotaja, sisi tunaendelea tutakutana mbele ya safari wakiwa tayari, wajumbe wake wapo Dodoma kwa ajili ya mkutano katika wajumbe 13 ni wawili tu ndiyo hawajathibitisha."

"NCCR-Mageuzi wanasema uongo, wanahadaa wananchi waeleze sababu haswa zinazowazuia kuhudhuria mkutano huu, CHADEMA msimamo wao upo wazi siku nyingi japo nao walishiriki kuandaa mkutano huu," alisema Kabwe.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema pia kuwa chama hicho hakitashiriki kongamano hilo, akidai kuwa lengo la kikao hicho ni maridhiano, lakini hawajawahi kukaa na kuangalia kwamba ni nini wanakitathmini katika suala hilo.

"Lakini kati ya watoa mada katika kongamano hilo ni Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, aliyeharibu uchaguzi ndiye anayeenda kuwaeleza jinsi ya kuwa na tume huru, kwa hiyo tukaona kwamba hatuna haja wala sababu ya kushiriki kongamano hilo," alisema Mrema.

Jana, Wakili na Mwanasheria NCCR-Mageuzi, Boniface Mwambukusi, wakati akizungumza na waandishi wa habari, alisema Kamati Kuu ya NCCR ilisikitishwa na mwenendo wa TCD, akieleza kuwa ndiyo wenye jukumu la kuandaa mkutano huo, ajenda na kuhakikisha maazimio na taratibu zinafuatwa jambo ambalo halikuzingatiwa.

Pia alisema hadi sasa TCD hawajakipatia NCCR-Mageuzi taarifa rasmi ya kichama kuhusu mkutano huo, kwamba wanaamini hata viongozi wengine wa kitaifa wanapotoshwa na kituo hicho.

"Kikao cha Dodoma ni maziwa yaliyoghushiwa hatuko tayari kuwapa Watanzania maziwa hayo, ajenda zinazojadiliwa ziliighushiwa, kikao kimoja kina ajenda tofauti, una lengo la kuwatega watakaohudhuria ili waweze kuidhinisha mambo ambayo ni kinyume na utashi, kuna mapendekezo yanapelekwa ya mabadiliko ya sheria ya vyama na uchaguzi, lakini vyama ambavyo vinatakiwa kuukubali muswada ule havijapatiwa mpaka dakika hii.

"Msimamo wa NCCR-Mageuzi ni kwamba hatutakuwa kamwe madalali wa demokrasia na haki za Watanzania, msingi wetu utajikita katika kuheshimu utu, mamlaka za kiuongazi na kukubali kupeana nafasi," alisema na kuongeza:

"Katika hali ya kuheshimiana, imani yetu tunaamini chama kilichoshinda kinawajibu wa kutovikwamisha na kuvizuia vyama vingine kujiandaa kwa ufasaha ili kuweza kushindana katika uchaguzi unaofuata."

Aliongeza kuwa kinachokwenda kufanyika Dodoma ni 'picnic' (mapumziko) na siyo kinachotarajiwa akidai kuwa kuna baadhi ya watu wanafanya utani na changamoto muhimu za kidemokrasia zinazowakabili Watanzania.

"NCCR-Mageuzi tunasema kwenye mradi huu hatuna bei, tunarudi kwenye msimamo wetu kwamba hatutashiriki mkutano wa Dodoma, siyo kwa sababu ya kiburi au jeuri ni kwasababu hatuwezi kwenda mnadani kufurahisha mtu, huku tukiwaumiza Watanzania kuanzisha na kuwa na chama ni mkataba, kushindwa kuwajibika kwa chama cha siasa ni usaliti kwa wananchi hatutakuwa sehemu ya usaliti huo," alisema Mwambukusi.

Aidha, alidai kuna baadhi ya watu wanataka kugombanisha vyama na serikali kwa maslahi yao binafsi, akisisitiza kuwa wanahitaji kuwa makini na nchi na hawatarudi nyuma na hawataishia kutoshiriki bali kamati kuu imesisitiza kwa uongozi wa chama taifa kukutana na vyama vingine kwa kusudio moja la kuhakikisha wana katiba bora na Tume Huru ya Uchaguzi kabla ya mwaka 2025.

Pia alisema azimio la chama hicho kuhusu mkutano wa Dodoma halikutekelezwa kwa kutokukutana na Rais wala hawajaandaa ajenda.

Alisisitiza kuwa kila jambo lina utaratibu na kudai kuwa TCD hawajazingatia utaratibu katika kuandaa mkutano huo.

Kwa mujibu wa mwanasheria huyo, kuna watu wanaitumia TCD kwa maslahi binafsi na alisisitiza kuwa hawatakubali itetereke, wala kugeuzwa jukwaa la kufanyia udalali wa kisiasa.

"Kamati kuu ya chama imeelekeza wajumbe wote waliokwisha kuanza safari wa NCCR-Mageuzi warejee walikotoka, hatutahudhuria wala hatutashiriki na wala hatutajifunga na chochote kitakachojiri mpaka pale taratibu za TCD zitakapozingatiwa na maelekezo tuliyokubaliana ya kuonana na Rais yatakapotekelezwa," alisema Mwambukusi.

"Maridhiano kwa taifa ni jambo la msingi, lakini ni suala la kujikita katika msingi wa kuaminiana na kuheshimiana, huwezi ukafanya maridhiano kwa ulaghai, ukisoma programu zinazoandaliwa humu ndani kuna vitu ambavyo siyo 'product' (zao) la TCD, lakini zinachomekwa kwenye mfumo wa kituo bila wahusika kuridhia," alisema Mwambukusi.

"Tunaamini katika maridhiano, umoja na ushirikiano, hata kushiriki kwetu kwenye 'technical committee' (kamati ya ufundi) ya TCD ilikuwa ni kuonyesha utayari wetu wa namna tunavyotaka kuonana, kuja karibu na wenzetu tukae kama watanzania, tutengeneze mfumo mzuri wa kisheria anayeshinda ashinde, anayeshindwa akubali kushindwa ajipange tena wakati ujao," alisema Mwambukusi na kuongeza:

"Hatutashiriki Dodoma na hatutakubaliana na kile kitakachoendelea kwa sababu hakijafuata taratibu, kanuni na matakwa ya mwongozo wa TCD unavyohitaji."

## Watalii wa Israel kumiminika nchini wiki hii

**Na Christina Mwakangale**

WATALII 961 kutoka Israel wanatarajiwa kuwasili nchini kuanzia Aprili 9, mwaka huu, huku ikielezwa kwamba utalii wa ndani umeongezeka kwa asilimia 40.2 kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 na kufikia 788,933 mwaka 2021.

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji Thomas Mihayo, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu hali ya sekta hiyo baada ya juhudi za kutangazwa vivutio kwa kushirikiana na wadau ikiwamo programu ya Royal Tour.

Jaji Mihayo alibainisha kwamba idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa asilimia 48.6 licha ya kuathiriwa na janga la UVIKO-19, akisema takwimu za watalii zinaonyesha 620,867 walifika nchini mwaka 2020 na mwaka jana ikiwa ni 922,692.

"Mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka Dola milioni 714.59 (sawa na Sh. trilioni 1.644), mwaka 2020 hadi kufikia Dola milioni 1,254.4 (sawa na Sh. trilioni 2.886) mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia 76.

"Tumeendelea kupokea watalii kutoka masoko yetu ya kimkakati yanayojumuisha Israel, wiki hii tunatarajia kupokea watalii 300 ambao watatembelea vivutio vya utalii na wengine 600 wanatarajiwa kuwasili Aprili 16, mwaka huu," alisema Jaji Mihayo.

Alibainisha kwamba bodi hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imelenga kufikia idadi ya watalii milioni tano ili kuliingizia taifa dola bilioni sita ifikapo mwaka 2025.

"Programu maalum ya Royal Tour katika mtandao wa habari nchini Marekani wa theGrio, umetambua juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuiongoza vyema sekta ya utalii na kuifanya Tanzania kuwa kivutio cha kwanza cha Utalii Afrika Mwaka 2022," alisema Jaji Mihayo.

## Mwigulu aomba sapoti wadau sekta ya mifugo

**Benny Mwaipaja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ametoa rai kwa wadau wa sekta ya mifugo nchini kuisaidia serikali kutimiza nia yake ya kuimarisha uzalishaji wa nyama na maziwa ili kuongeza tija na kukuza uchumi wa nchi na maendeleo ya watu.

Dk. Nchemba alitoa rai hiyo jijini Dodoma, alipokutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, wataalamu kutoka wizara hiyo na Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na wazalishaji binafsi katika sekta za maziwa na nyama nchini.

Alisisitiza kuwa sekta ya mifugo itakuwa na mchango mkubwa katika kukuza kipato cha wananchi hususan vijana, lakini itaongeza mapato ya nchi kwa kuzalisha bidhaa za nyama na maziwa zitakazouzwa ndani na nje ya nchi hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni.

Aliwataka wadau hao kuwa walimu wa kuwaongoza na kuwafundisha vijana namna ya kuzalisha mifugo bora kwa ajili ya nyama na maziwa na kwa kuwa wana mtandao wa masoko, ni rahisi kwa wafugaji kupata maeneo ya kuuza mazao yao.

Dk. Nchemba, alitoa wito pia kwa vijana na wawekezaji kuchangamkia fursa zinazopatikana katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili wajipatie ajira katika sekta hizo muhimu badala ya kuwaachia wazee peke yao kujihusisha na masuala ya kilimo na mifugo na kuahidi kuwa serikali iko tayari kuwawezesha maeneo na mitaji.

Naye Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliwahakikishia wadau hao wanaomiliki kampuni na viwanda vya kusindika nyama na maziwa kwamba serikali iko tayari kushirikiana nao kuboresha sekta ya mifugo ili ilete tija nchini.

Aidha, alisema kuwa fedha zitakazoongezwa na serikali katika Bajeti Kuu ya Mwaka 2022/2023 katika Wizara yake, zitaelekezwa kwenye maeneo yenye kuongeza uzalishaji ili kukuza ajira kwa vijana pamoja na kuzalisha mazao yatakayokuza mauzo nje ya nchi.

Kwa upande wao, wadau wa sekta ya mifugo walioshiriki kikao hicho, wameishauri serikali kukuza sekta ya mifugo kwa kuwekeza kwenye masuala ya vipaumbele ikiwamo uhimilishaji, kuongeza huduma za ugani, afya ya mifugo na kujenga miundombinu ya kuchakata bidhaa za mifugo na kutafuta masoko ya uhakika.

# Wachangishwa 10,000/- wasihamishwe Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

BAADHI ya wananchi wanaoishi eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) wamesema 'kiburi' walichonacho viongozi wa vijiji, wazee wa mila wa jamii ya wafugaji wa Kimasai na baadhi ya wanasiasa, kinatokana na kuwachangisha fedha wakazi ili kwenda kuwatetea wasiondolewe hifadhini.

Wamesema viongozi hao huwachangisha wanawake Sh. 2,000 na wanaume Sh. 10,000.

Madai hayo yalifichuliwa juzi na wawakilishi wa wananchi wanaotaka kuhama kwa hiari kwenda Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga.

Akizungumzia michango hiyo, mwakilishi wa wananchi wa Kata ya Endulen, Foibe Lukumay alisema: "Mikutano kila siku na kuchangishwa hao hao wanachangishwa. Hata mimi nimechanga kwa sababu ni mwanakijiji.

"Kwa nini nisichange kama tukiambiwa na viongozi wenzetu wa mila kwa ajili ya kwenda kutetewa. Wanawake wa Kimasai, hawana nguvu na hawana haki kwa mume, kusema kwamba mimi nitaondoka wewe ubaki, haiwezekani.

"Tunachangishwa ili viongozi waondoke kwenda kutusaidia, hasa Malaigwanani (wazee wa mila), kama wanaweza kufika hata kwa mama yetu Rais Samia Suluhu Hassan."

Foibe, ambaye ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Endulen, alisema wanawake lazima watoe mchango huo kwa sababu wako chini ya wanaume.

Aidha, kwa sasa katika Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na masuala ya utoaji elimu ya kujitambua, kujikwamua kiuchumi na haki za jamii za kifugaji, yanatajwa kufanya kampeni za chini kwa chini kushawishi wananchi wasiondoke kwenye makazi yao wanayodai ni ya asili.

Mwanaharakati na Mkazi wa Kitongoji cha Irmuli, Kijiji cha Oloirobi, Kata ya Ngorongoro Paulo Mamasita, alisema: "Ninavyoona mimi ni kama wanafaidika kupitia mchakato huu. Ile kwenda kushawishi wao wanapata fedha kwa wafadhili, hawajui wanamuumiza yule mtu wa hali ya chini, kwa sababu yule hajasoma, hawezi kuona vitu kwa mapana zaidi kama yeye".

Alisema wananchi wanaotaka kuhama kwa hiari Ngorongoro, wanasumbuliwa, hivyo wanashindwa kutoa maamuzi ambayo ni sahihi.

Hivyo, aliiomba serikali iyachunguze mashirika hayo pamoja na baadhi ya watu binafsi wanaotumia ushawishi wao kuvuruga zoezi hilo.

Kiongozi wa Mila wa Jamii ya Kifugaji ya Kimasai (Laigwanani), Matengwai Ole Tauwo, Mkazi wa Kijiji na Kata ya Aleilai alisema:

"Nimeona Ngorongoro hakuna kitu cha kutawala, hakuna miliki ya ardhi, hakuna ruhusa ya kuvuna miti au kufanya maendeleo yoyote ya kiuchumi. Ukitaka kwenda kwenye maeneo yenye maji ya kunywesha ng'ombe au mbuzi lazima utoe taarifa na ukitaka kupitisha pikipiki hairuhusiwi. Sasa kwa nini nikae Ngorongoro".

Mkazi wa Ngereiyani, Kijiji cha Osinoni, Kata ya Kakesio, Lukas Tiamasi, alisikitishwa na kauli za baadhi ya wanaharakati wanaotoa elimu ya ushawishi kwa wananchi ili wasihame.




Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Evarlasting Lyaro, akitoa maelezo kuhusu kazi za mamlaka hiyo kwa mgeni aliyetembelea banda hilo wakati wa kongamano la Sayansi na Maji jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NHC kujenga nyumba za wenye kipato cha kati Dar na Dodoma

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limetaja vipaumbele 11 vitakavyoanza kutekelezwa hivi karibuni, ukiwamo ujenzi wa viwanda vya vifaa vya ujenzi vya shirika hilo pamoja na kujenga nyumba za makazi 360 eneo la Kawe mkoani Dar es Salaam, na pia 1,000 zitajengwa Dodoma maalumu kwa wakazi wenye kipato cha kati.

Limesema kipaumbele kingine ni kukamilisha miradi ya Morocco Square na Kawe 711 iliyoko jijini Dar es Salaam, ambayo ilisimama tangu mwaka 2018 kutokana na upungufu wa fedha na kwamba serikali imeidhinisha shirika hilo kukopa Sh. bilioni 173 ili kumalizia miradi hiyo.

Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, alibainisha vipaumbele hivyo jana mkoani Dar es Salaam alipokuwa akizungumzia mwelekeo mpya wa shirika baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kumteua Nehemiah Mchechu kuwa Mkurugenzi Mkuu.

Alisema gharama kubwa za vifaa vya ujenzi ikiwamo mabati, nondo, kokoto na nondo zinasababisha majengo ya NHC kupangishwa au kuuzwa kwa bei kubwa na kwamba ujenzi wa viwanda vya shirika vitakavyogharimu Sh. bilioni 12 ili kupunguza gharama hizo, huku akibainisha kwamba uzalishaji wa viwanda ukitosheleza mahitaji ya shirika, watauziwa watu wengine.

Saguya alibainisha kwamba ujenzi wa nyumba za makazi utaanzia mkoani Dar es Salaam kwa kujengwa nyumba zipatazo 360 eneo la Kawe, maalumu kwa ajili ya watu wa kipato cha kati na pia eneo hilo kutajengwa maduka ya biashara.

"Nyumba hizi zitajengwa Kawe, jirani na Tanganyika Packers na zitauzwa kati ya Sh. milioni 90 hadi 150. Pia maeneo mengine ya nchi zitajengwa nyumba na kuuza na kupangisha kwa kutumia ardhi nafuu, hata kwenye eneo la mipaka ya nchi tutajenga majengo makubwa ya biashara," alisema Saguya.

Pia alisema kwamba shirika litashirikiana na wadau mbalimbali katika ujenzi wa miradi hususan miundombinu ya maji, barabara na umeme kwenye maeneo ya ujenzi, kadhalika NHC itaendelea kusimamia na kuboresha miliki zake za nyumba 18,622 zilizoko nchi nzima, kwa kuzifanyia matengenezo ya paa, vyoo na madirisha chakavu na zimetengwa Sh. bilioni 50.

"Shirika linaendelea kukusanya madeni ya kodi ya nyumba yanayofikia Sh. bilioni 22 yatokanayo na uuzaji nyumba, viwanja. Msisitizo utakuwa anayedaiwa deni atalipa deni, ili kuwezesha shirika kuendelea kuwahudumia Watanzania wote," alisema Saguya.

Saguya alisema kwamba mkoani Dodoma utaendelea ujenzi wa majengo manane ya wizara mbalimbali katika mji wa Mtumba ambayo hadi kukamilika itatumia Sh. bilioni 186.83 huku ujenzi wa awamu ya tatu nyumba za makazi maeneo ya Medeli na Iyumbu mkoani Dodoma, ukitarajia kukamilika baada ya kupatikana ardhi ya uendelezaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada zinahitajika sasa kutunza misitu endelevu

**WATAALAMU** na wadau wa misitu wiki iliyopita walikutana kushirikishana uzoefu na taarifa kuhusu changamoto na fursa zilizoko kwenye utunzaji na uhifadhi endelevu wa misitu katika wakati wa mabadiliko ya tabianchi.

Kwenye mkutano huo ilielezwa kuwa hekta milioni 3.9 za misitu Afrika, hupotea kila mwaka hutokana na wadudu, magonjwa, moto na shughuli za kibinadamu, huku wakitaka jitihada za makusudi za serikali za nchi kuokoa raslimali hiyo.

Jukwaa la Misitu Afrika (AFF), ndilo liliandaa mkutano huo ambao hufanyika kila mwaka kuangalia hali halisi ya misitu, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, changamoto na kuzishauri serikali za nchi husika.

Kila nchi ina sera na sheria nzuri za misitu lakini changamoto kubwa ni kuzisimamia ili zifanye kazi hadi ngazi ya chini kabisa, ambako ndiko wanajamii wanaishi na wanahusika na misitu moja kwa moja.

Wengi hudhani misitu inaota yenyewe, haihitaji kutunzwa na kulindwa, lakini hawafahamu umuhimu wake katika kuondoa hewa ukaa na kuchangia mazingira mazuri kwa ajili ya wanadamu na viumbe vingine.

Misitu husaidia kuondoa hewa chafu na kutoa hewa safi, huboresha mwonekano mzuri wa mazingira yetu, husaidia kupatikana kwa maji, mvua na kutunza uoto wa asili, huvutia wanyama na viumbe wengine lakini kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Misitu husaidia kupatikana kwa dawa mbalimbali, huku asilimia kubwa ya dawa za hospitalini zinazotengenezwa zinatokana na misitu, pia kwenye misitu hufanyika shughuli za kimila kama matambiko ya makabila mbalimbali. Aidha, mazao ya misitu husaidia kupata mbao ambazo hutumika kuitengeneza samani na bidhaa nyingine, pia ni biashara inayoliingizia taifa fedha ambazo hutumika kwenye miradi ya maendeleo na huwezesha wananchi kurina asali.

Kasi ya kuvuna misitu kwa ajili ya biashara na matumizi ya nyumbani ni kubwa, huku ya kupanda, ikiwa ndogo jambo ambalo ni hatari kwa ustawi wa maisha ya viumbe wote.

Ukikata mti leo na kupanda mwingine itachukua miaka mingi kukua na kufikia uliokatwa kwa ajili ya mkaa, ndiyo maana wananchi wanaelimishwa na serikali inawajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa nishati mbadala ili waachane na kutegemea misitu.

Wapo wananchi ambao wanategemea misitu kuendeleza maisha yao kwamba watarina asali, watavuna mbao na mikaa kisha wapata kipato, ni lazima kuwaelimisha umuhimu wa kutunza raslimali hiyo hasa wakati wa mabadiliko ya tabia nchi ili iwe endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho. Aidha, wataalamu hao wamebaini kuwa changamoto wadudu waharibifu, magonjwa ya miti ya misitu na matukio ya moto kutokana na shughuli za kibinadamu ni changamoto nyingine, ambayo inapaswa kuangaliwa kwa jicho la pekee.

Tanzania kuna mashamba ya miti, misitu ya mikoko, mashamba ya nyuki na misitu ya asili ambayo yote iko chini ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), ambaye dira kuu ni kwa kielelezo bora katika usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu na nyuki, huku dhima ni kuwa na usimamizi endelevu wa raslimali za kitaifa za misitu na nyuki ili kuchangia mahitaji ya kijamii, kiuchumi, ki-ikolojia na kiutamaduni kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Ni muhimu wadau wote kushirikiana kuangalia kwa karibu sera na sheria zilizoko kama zinatekelezwa ipasavyo hasa kwa wakati wenye mabadiliko makubwa ya hali ya tabia nchi, kuhakikisha wananchi wanashirikishwa na kuwa sehemu ya walinzi wa raslimali hiyo.

Mathalani, kuna changamoto kubwa inayokuwa kwa kasi ya udongo wenye rutuba kuzolewa kutoka mlimani kwenda bondeni kutokana na kilimo kisicho cha kisasa, maana yake tabaka la ardhi linalobaki ni ambalo halina rutuba.

Ni lazima kuangalia kwa karibu kama sera na sheria zilizoko zinakwenda na uhalisia, lakini kuwashirikisha wananchi kutambua na kutatua changamoto za misitu na mazingira kwa ujumla kwa uhalisia ili kuhakikisha misitu inatunzwa na kuwa endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Elimu iwe zaidi kuliko faini kukabili ajali za barabarani

**Imekuwa kawaida kusikia ajali imetokea huku chanzo chake kikitajwa kuwa ni uzembe wa madereva na kama ndivyo, basi badala ya kukazania kuwatoza faini, mkazo zaidi uwe ni kuwaelimisha ili waone umuhimu wa kubadilika.**

**MWEZI** Machi umeisha ikiwa umeangamiza roho za baadhi ya watu kutokana na ajali za barabarani zilizotokea ndani ya mwezi huo, katika mikoa mbalimbali ikiwamo Morogoro, Simiyu, Tanga na Pwani.

Ajali hizo ni mfululizo wa zile zilizotokea tangu kuanza kwa mwaka huu wa 2022, hali ambayo nadhani kwamba sasa kuna haja ya kuwapo elimu ya kutosha kwa madereva na watumiaji barabara na abiria kwa ujumla.

Inasikitisha kuona ajali hizo zikiendelea kuleta simanzi kwa Watanzania kutokana na ukweli kwamba, zinaondoa nguvu kazi ambayo ni tegemeo kwa familia na kwa maendeleo ya nchi.

Ingawa siku za nyuma ni kama zilianza kupungua kwa kiwango kikubwa, lakini ghafla zimeibuka kwa kasi ndani ya kipindi kifupi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

Askari wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, wamekuwa wakifanya kazi nzuri kukabiliana na madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani, hata kuwapa adhabu waogope na kufanya kazi yao kwa umakini.

Hata hivyo, inaonekana wapo baadhi ya madereva ambao bado wamekuwa wagumu kuzingatia sheria hizo na badala yake kuendelea kusababisha ajali zinazogharimu maisha ya watu wasio na hatia.

Ninaamini, bado madereva wengi wanaendelea kufanya makosa wawapo barabarani, hali inayoonyesha kuwa ipo haja ya kuwekeza nguvu katika utoaji wa elimu, ili kuwasaidia wabadilike.

Kwanini? Kitendo cha Jeshi la Polisi kukusanya faini ya Sh. bilioni 50.1 kama faini kutoka kwa madereva wanaofanya makosa ndani ya kipindi cha miezi 10, ni wazi elimu zaidi inahitajika kuliko faini.

Hiyo ni taarifa ya Mkuu wa Jeshi la Polisi IGP Simon Sirro aliyoitoa Mei mwaka jana, kwenye uzinduzi wa kiwanda cha ushonaji katika bohari kuu ya jeshi hilo kilichoko eneo la Kurasini jijini Dar es Salaam.

Kikosi cha Usalama Barabarani, kinafanya kazi nzuri, lakini pamoja na hayo, ninadhani ukusanyaji wa fedha nyingi za faini uwe kiashiria kuwa hatua zaidi zinatakiwa kuchukuliwa ili kupunguza makosa yanayoweza kusababisha ajali.

Makusanyo ya fedha za faini zitokanazo na makosa mbalimbali ya barabarani yanapopungua, ni wazi kwamba elimu imewaingia vizuri, lakini yanapokuwa makubwa, hiyo inatosha kuelewa kuwa elimu zaidi inahitajika.

Kukusanya fedha nyingi za faini za makosa mbalimbali ni wazi kwamba usalama barabarani nao ni mdogo na inawezekana baadhi ya vyombo vya moto vilivyoko barabarani havistahili kuwapo.

Inawezekana madereva wa vyombo hivyo, hawajui sheria za barabarani, hivyo kwa mantiki hiyo, suala la utoaji wa elimu ya kutosha kwa watu hao ni muhimu kunusuru maisha yao na abiria.

Hivyo, ukusanyaji fedha nyingi zinazotokana na faini za makosa mbalimbali ninaliona kama ishara ya kuwapo tatizo.

Pia ni wazi fedha nyingi za faini zinapokusanywa kutokana na makosa mbalimbali ni wazi usalama barabarani nao ni mdogo, ina maana kuna uwezekano baadhi ya vyombo vya moto havistahili kuwapo barabarani.

Imekuwa kawaida kusikia ajali imetokea huku chanzo chake kikitajwa kuwa ni uzembe wa madereva na kama ndivyo, basi badala ya kukazania kuwatoza faini, mkazo zaidi uwe ni kuwaelimisha ili waone umuhimu wa kubadilika.

Nieleweke kuwa sipingi faini, bali waendelee kutozwa, lakini elimu inaweza kuwabadilishia hatua, kwani nguvu kubwa ikiwa kwenye faini wanaweza kuendelea kusababisha ajali wakijua watalipa faini na kisha madereva wanaendelea na tabia yao.

Kwa mfano, wapo baadhi ya madereva ambao hutumia kilevi kisha wakaendesha vyombo vya moto hali ambayo ni hatari kwao na hata kwa abiria, hivyo ingekuwa ni vyema wakaelimishwa kikamilifu.

HABARI KITAIFA

## Bashe akiri uhaba wa mafuta ya kula

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema nchi inachangamoto ya upatikanaji wa mafuta ya kula na wizara inafanya jitihada kuhakikisha tatizo hilo linakwisha.

Bashe aliyasema hayo jana jijini Dodoma katika hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa vitendea kazi kwa maofisa ugani kilimo ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais Samia Suluhu.

Alisema kuwa Wizara ya Kilimo imeamua kufanya tathmini ya kina ili kuelewa wanahitaji nini ili kuondoa tatizo la uhaba wa mafuta wakati nchi ikiwa na mazao makuu mawili, mchikichi na alizeti.

"Mheshimiwa Rais, umetoa maelekezo kwamba tuhakikishe tunalitatua tatizo la mafuta uhitaji wa mafuta nchini ni wastani wa tani 650,000 kwa mwaka, uzalishaji wa ndani hauzidi tani 270,000, 'tunagape' ya karibu tani 400,000," alisema.

Katika kutatua taizo hilo wizara imegawa miche ya michikichi zaidi ya Sh. milioni 5 na kubadilisha mfumo wa kilimo kwa kuwaweka wakulima wa mfumo wa mashamba makubwa tu ikiwamo kampuni ya Wilma waliopatiwa hekta 10,000 Kigoma kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha mawese.

Alisema kwa upande wa alizeti changamoto kuu ilikuwa ni gharama kubwa ya mbegu ambayo ya Sh. 35,000 ambapo wizara imefanya majaribio kwa kugawa tani 2,000 za mbegu hiyo kwa mikoa mitatu na kuiuza kwa Sh. 3,500.

Aliongeza kuwa mwakani wanampango wa kuongeza tani za 5,000 za mbegu zilizothibitishwa kwa wakulima ili walime zao hilo na kuiomba Wizara ya Fedha pamoja na mambo mengine wapunguze kodi kwenye mafuta yanaoingia na kufuta kodi ya ongezeko la thamani kwenye viwanda vya ndani ili kuvifanya viwe vya ushindani.

Alisema licha ya sekta ya kilimo kuwa na umuhimu katika nchi ikiwamo kuajiri asilimia 62 ya nguvu kazi na kuchangia pato la taifa kwa asilimia 2.8, na asilimia 65 ya malighafi za viwandani lakini inakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Alisema kuwa sekta ya kilimo ni biashara na haiwezi kuleta tija na kumnufaisha mkulima kubadilika bila kuchukua hatua katika mambo ya msingi.

Alisema pia kwa muda mrefu thamani ya bidhaa zinazouzwa nje imekwamia kwenye wastani wa dola milioni 800 mpaka dola bilioni 1.2, huku akisisitiza kuwa sekta hii ikianguka na pato la taifa linaanguka.

Aliongeza kuwa Tanzania ina hekta milioni 44 inayofaa kwa kilimo huku milioni 29.4 ikifaa kwa umwagiliaji huku asilimia ndogo tu ndio inayotumika.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwaongezea bajeti utafiti kutoka Sh. bilioni 7 hadi 11 huku akisema hilo ni mojawapo muhimu yenye kuleta tija katika kilimo ikiwamo elimu, pembejeo za kilimo, huduma za ugani na miundombinu sahihi ya umwagiliaji.

# NMB yatoa bil. 8/- za mikopo ya riba nafuu kwa wakulima

**Na Mwandanishi Wetu,** DODOMA

JUMLA ya Sh. bilioni 8 zimeshatolewa na Benki ya NMB kwa wakulima kati ya Sh. bilioni 100 walizotengewa kwa ajili ya kukopeshwa kwa riba nafuu ili kusaidia kukuza mnyororo wa kilimo.

Fedha hizo ni sehemu ya mkakati wa Benki ya NMB kwa ajili ya sekta ya kilimo inayoajiri Watanzania wengi zaidi ambapo benki inatoa fedha hizo kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mpozi, wakati akimkaribisha Rais Samia Suluhu Hassan alipotembelea banda la benki hiyo.

Kwa upande wake Rais alipongeza juhudi zote zinazofanyika ndani ya benki hiyo akisema kuwa anawashukuru sana kwa juhudi zao hizo.

Rais Samia alifika katika banda hilo kwenye hafla ya ugawaji wa vitendea kazi kwa maofisa ugani nchi nzima ambayo ilifanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Mponzi alisema kati ya shilingi bilioni 100 zilizotengwa kukopeshwa kwa wakulipa kwa riba ya chini ya asilimia 10, zaidi ya shilingi bilioni 78.8 zimeshakopeshwa kwa wanufaika 3,773 huku wakiwafikia zaidi ya wakulima na wajasiriamali wa kilimo milioni 1.4 kupitia taasisi yao ya NMB Foundation.

"Mbali na kiwango hicho, pia Benki ya NMB imefanikiwa kuandaa mpango wa kufungulisha akaunti kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ambapo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita zaidi ya akaunti 500,000 zilifunguliwa," alisema Mponzi.

Ofisa huyo alisema lengo la njia hiyo ni kuwawekea wakulima utaratibu maalumu ili wakidhi vigezo vya kupatiwa huduma za kifedha ikiwamo mikopo na mafunzo.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, mpango huo ni kuunga mkono juhudi za serikali, katika kusukuma mbele ajenda ya maendeleo ya kiuchumi ya vijana na wanawake, hivyo waliamua kutangaza hati fungani maalumu tuliyoiita 'JASIRI BOND'. Hati hiyo imejikita katika kuwasaidia wanawake wajasiriamali kwa riba nafuu ambapo mwitikio umekuwa mkubwa sana, hivyo kuamua kuzindua NMB PESA lengo likiwa ni kurahisisha huduma za kipesa kwa wakulima na wateja wote kuwa karibu zaidi kwenye maeneo yao.

Akizungumzia utoaji wa mbegu za mafuta, alisema tayari wateja 332 wakiwamo wakulima katika vyama vya ushirika (AMCOS) wameshanufaika na zaidi Sh. bilioni 6 zimetolewa kwenye eneo hilo kama mikopo.

Nyingine ni kuwa benki hiyo imeshatoa zaidi ya Sh. milioni 110 kama mikopo ya bima ya afya kwa makundi na taasisi za wakulima 697.

Kwenye sekta ya mikopo NMB kwa kipindi cha miaka mitano wameshakopesha zaidi ya Sh. trilioni 1.3 kwenye kilimo, uvuvi na ufugaji na minyororo yote ya thamani.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa mpango wa kulinda vijana kiafya na kuwawezesha kimaendeleo uitwao Safeguard Young People Programme (SYP), ambao unafadhiliwa na Serikali ya Uswisi kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Uzio wa chuma kujengwa Ziwa Rukwa kudhibiti mamba

**Na IbrahimYassin,** SONGWE

KUTOKANA na idadi kubwa ya mamba wanaozidi kula watu na kuzua hofu kwa wakazi wa mwambao wa Ziwa Rukwa wilayani Songwe mkoani Songwe, serikali imeanza mikakati ya kujenga uzio na vizimba kuondoa kadhia hiyo sambamba na utaratibu wa kuvuna mamba ukifanyika.

Ziwa Rukwa ni miongoni mwa maziwa yanayotajwa kuwa na idadi kubwa ya mamba ambao wanazaliana siku hadi siku huku idadi ya watu kuliwa na wengine kujeruhiwa wakiwa majini kuvua samaki ama kuchota maji pembezoni mwa ziwa ikiongezeka.

Miaka ya nyumba katika Forodha ya Manda Kata ya Udinde wilayani idadi kubwa wamekuwa wakifa kwa kuliwa na mamba na wengine kujeruhiwa wazazi wa Mbunge wa Jimbo hilo, Fillipo Mulugo.

Makani Sande, mkazi wa Udinde, alisema kutokana na idadi kubwa ya watu kufa kwa kuliwa na mamba wakiwamo wazazi wote wawili wa Mulugo, waliiomba serikali kwa nyakati tofauti kufanya utaratibu wa kuvuna mamba ili kupunguza vifo pasipo mafanikio.

"Tunaomba serikali itimize mpango wa kuvuna mamba, hata Mbunge Mulugo amekuwa akisisitiza hilo kwa nyakati tofauti akiwa bungeni, mamba ziwani ni wengi na wana njaa inafikia hatua wanawarukia wavuvi wakiwa ndani ya mtumbwi," alisema Sande.

Asale Mwashihuya mkazi wa kijiji cha Manda, alisema kutokana na vifo na majeraha mengi yaliyotokana na watu kukamatwa na mamba, viongozi wengi wakiwamo mawaziri wenye dhamana walifika na kuahidi kuwavuna mamba, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea.

Alisema mwaka juzi aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamis Kigwangala alifika maeneo hayo na kuahidi kufanya utaratibu wa kuwavuna mamba ili kupunguza vifo, lakini ikawa ni hadithi watu bado wanaendelea kufa na wengine kupewa ulemavu.

Hata hivyo, Ofisa Maliasili, Misitu na Utalii wilayani humo, Abdallah Mgonja, alisema ni kweli ziwa hilo lina mamba wengi, kwamba serikali inajipanga kuwavuna mamba hao, na kuwezesha ujenzi wa uzio wa chuma pembezoni mwa ziwa ili mamba wasiendelee kuwakamata watu.

Aliiambia Nipashe kuwa katika uzio huo, wanajenga vizimba vitakavyokuwa na mlango ambapo watu watakapoenda kuchota maji, mamba wakiwafuata hawataweza kuwafikia, hivyo kupunguza hali hiyo itapunguza wimbi la vifo.

Alisema maeneo yale ni hatari lakini watu hawataki kuhama kwa sababu shughuli zao ni uvuvi ambazo huendesha maisha yao ya kila siku.

# Bodi ya Nafaka yatoa suluhisho ongezeko la bei

**Na Richard Makore,**
MWANZA

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iliyoko chini ya Wizara ya Kilimo Kanda ya Ziwa, imejitosa kuzalisha kwa wingi vyakula mbalimbali ili kukabiliana na ongezeko la bei katika kipindi cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana jijini hapo, Meneja wa Bodi hiyo, Steven Kubona, alisema, wameanza kuzalisha mchele na unga wa sembe katika kiwanda chao kilichoanza kufanya kazi hivi karibuni jijini humo.

Vile vile, alisema wanauza maharagwe, korosho, dengu, ufuta pamoja na mazao mengine wanayoyanunua kutoka kwa wakulima vijijini ili kuhakikisha jamii inauziwa kwa bei nafuu.

"Mwezi kama huu wafanyabiashara wengi wanapandisha bei za vyakula, lakini sisi tumeamua kuja kitofauti kwa kuwa tunanunua mpunga kutoka kwa wakulima na kuukoboa wenyewe ukiwa na viwango vya hali ya juu na kisha kuwauzia wananchi kwa bei nafuu," alisema.

Aidha, alisema mazao wanayokoboa wanauza kwa wananchi mmoja mmoja na jumla hatua ambayo inalenga kuwapunguzia mzigo wa bei kubwa Watanzania waliopo Kanda ya Ziwa na maeneo mengi ya nchi.

Kuhusu kumwinua mkulima, Kubona alisema wamefungua milango kwa wakulima wote wa mpunga kuuza mazao yao kwao na kwamba hawahitaji kuwa na dalali.

Alisema lengo ni kuhakikisha mkulima anainuka kiuchumi na kwamba kiwanda chao bado kina uhitaji mkubwa wa malighafi ikiwamo mahindi na mpunga.

Aliongeza kuwa wanatoa kipaumbele kwa wakulima wadogo wa mpunga na mahindi na kwamba kila mtu atakayefikisha mzigo wake kwao atalipwa fedha siku hiyo hiyo na kuondoka.



Waziri wa Uingereza anayeshughulikia masuala ya Afrika, Latini Amerika na Caribbean, Vicky Ford (katikati), akipewa maelezo kuhusu bidhaa za SBL na Meneja wa Kiwanda cha Moshi, Alice Kilembe (kushoto), alipotembelea kiwanda cha bia cha Serengeti Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TASAF ilivyobadilisha maisha ya Tunduru

**Na Gideon Mwakanosya,** TUNDURU

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wameeleza namna mfuko huo ulivyobadilisha maisha yao ikiwamo kununua mashamba, mifugo pamoja na kusomesha watoto.

Wakizungumza na Nipashe jana katika Kijiji cha Mbesa, wanufaika hao wamesema licha ya mfuko huo kuwaletea maendeleo lakini wameomba kuongezewa fedha, kwamba wanacholipwa kwa sasa ni kidogo na hakikidhi mahitaji yao.

Mmoja wa wanufaika hao Mwanahawa Ngunga (57) kutoka Kitongoji cha Mnyangwe alisema licha ya TASAF kuendelea kumsaidia, ana watoto wanne ambao wanasoma Shule ya Msingi Mbesa na wengine sekondari ambao wanamtegemea.

Alisema awali alikuwa analipwa Sh. 48,000 kila baada ya miezi mitatu, lakini kwa sasa kiwango hicho kimepunguzwa hadi Sh. 36,000.

Mwananchi mwingine Saidi Athumani Kapilima, kutoka kitongoji cha Mkanyageni alisema baada ya kuanza kupatiwa msaada wa fedha kupitia TASAF alianza kulipwa Sh.36, 000 kati ya fedha Sh. 20,000 alizitenga kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wanne kwa kuwanunulia madaftari na sare za shule na Sh. 16,000 aliweka akiba.

Alisema baada ya mwaka mmoja alikuwa na Sh.150,000 ambazo zilimwezesha kununua shamba la korosho hekari nne.

Kapilima alisema mafanikio aliyoyapata kutokana na kulipwa fedha kutoka TASAF mojawapo ni kumsomesha mtoto wake Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam anasomea Shahada ya Ualimu.

Alisema watoto wake wengine watatu wanasoma katika Shule ya Sekondari ya Mbesa, pamoja na kufuga kuku wa kienyeji zaidi ya 40.

Mkazi wa Kitongoji cha Mchangani, Amina Ally Athumani, alisema TASAF imemnufaisha kuwa na nyumba ambayo hivi sasa anaishi na ndugu zake.

Mratibu wa TASAF wilayani Tunduru, Mhidini Shaibu, alisema miradi 148 ya ajira za muda imetekelezwa wilayani Tunduru kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Alitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni uboreshaji wa visima, ujenzi wa barabara za mitaa, upandaji wa miti ya matunda, ujenzi wa vivuko na mabwawa ya kuhifadhia maji.

# CRDB, NIDA kuwafikishia wananchi vitambulisho

**Na Mwandishi Wetu,**
RUANGWA

BENKI ya CRDB kupitia tawi lake la Ruangwa mkoani Lindi imeendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha kila Mtanzania anapata Kitambulisho cha Taifa.

Hivi karibuni benki hiyo kupitia tawi la Ruangwa, ilianza kuwatembelea wateja wao na kuwafungulia akaunti wateja wapya wakiwa wameambatana na maofisa wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kuwahamasisha wananchi wilayani humo kujipatia vitambulisho vyao.

Akizungumzia utaratibu huo, Msimamizi wa Uandikishaji NIDA, wilayani Ruangwa, Khalaf Mwalimu, alisema lengo ni kuhakikisha kila mwananchi anapata kitambulisho.

"Tunaishukuru Benki ya CRDB tawi la Ruangwa kwa ushiriki wao katika kuisaidia mamlaka hasa katika wilaya yetu ya Ruangwa katika kufanikisha usambazaji wa vitambulisho vya taifa na usajili mpya wa wananchi waliokuwa bado hawajajisajiliwa na NIDA," alisema. Awali, Meneja Huduma kwa Wateja wa Benki ya CRDB tawi la Ruangwa, Mwichande Mwichande, alisema kupitia kampeni hiyo wanaitangaza akaunti ya Fahari Kilimo ambayo ni maalumu kwa wakulima nchini wameweza kuwafikia wananchi wengi kupitia ushirikiano walioufanya na NIDA wakati wa zoezi la usajili na ugawaji wa vitambulisho.

"Kampeni hii imetusaidia kuongeza wateja wapya katika tawi letu kwa wale wananchi waliokosa fursa ya kufungua akaunti kwa kuwa hawakuwa na namba za NIDA," alisema Mwichande.

Naye Ofisa wa Huduma na Mauzo wa CRDB Tawi la Ruangwa, Jesca Kapelo, alisema kupitia kampeni hiyo walitembelea Naunambe, Mbekenyera, Chibula, Mandawa na Nandagala.

Naye Ofisa Mauzo (DSE) wa benki hiyo, Yusuph Masoud, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kusajiliwa kwa ajili ya kupewa vitambulisho hivyo kwenye maeneo ambako zoezi hilo linaendelea ili kutoa fursa kwa kila mwananchi mwenye sifa kupata kitambulisho.

# W'biashara wa chumvi watakiwa kufuata viwango

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAZALISHAJI na wauzaji wa chumvi kisiwani Pemba wametakiwa kuhakikisha chumvi wanayozalisha inakuwa na madini joto kwa kiwango kinachotakiwa, ili kulinda usalama na afya ya mlaji.

Akifungua mkutano kwa wazalishaji na wauzaji chumvi huko Gombani Chake chake, Mkuu wa Idara ya Kinga na Elimu ya Afya Pemba, Khamis Bilal Ali alisema ni vyema wajasiriamali hao wakasaidia kusukuma gurudumu la afya mbele.

Alisema kuwa wajasiriamali hao wahakikishe chumvi wanayozalisha inakuwa na madini joto, ili kuwalinda watumiaji dhidi ya magonjwa yatokanayo na ukosefu wa madini joto, ikiwamo goita.

"Mashamba ya chumvi yanaongezeka siku hadi siku, hivyo ni lazima msimamiwe vizuri kuhakikisha watumiaji wanakuwa salama na kuwakinga na magonjwa mbalimbali ikiwemo goita," alisema.

Kwa upande wake, Mratibu Kitengo cha Lishe Pemba, Raya Mkoko Hassan alisema, Serikali imeridhia maadhimio ya Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kupambana na kutokomeza madhara yatokanayo na madini joto, hivyo juhudi zinahitajika kuhakikisha wazalishaji na wauzaji wanasaidiwa.

# Prof. Janabi: Chanjo ya UVIKO-19 ni salama

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wanaosita kupata chanjo ya UVIKO-19, wakihofia usalama wake, wamekumbushwa kuwa nchi ina uwezo wa kudhibiti dawa na bidhaa zote za matibabu zinazoletwa nchini, hivyo wajitokeze kwa wingi kuchanjwa. Akizungumza kituo kimoja cha redio mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Prof. Mohammed Janabi, alisema Watanzania hawapaswi kuhofia chanjo hiyo.

"Nchi ina uwezo huo, ndio maana tunahakikishiwa kuwa chanjo hizi ni salama, hivyo suala la utasa na mengine ambayo yamekuwa yakihisiwa kuhusu chanjo hayapo," alisema.

Alisema madai hayo na mengine kuhusu chanjo hiyo, hayana uthibitisho wa kisayansi, na kuongeza kuwa, iwapo mtu anataka kuthibitisha kuwa chanjo inaweza kusababisha ugumba, lazima kuwe na ushahidi unaohusisha mtu kuchanjwa na kujaribu kushika mimba katika mwaka wa kwanza, wa pili au wa tatu, na kwamba hatua hiyo inapaswa kufuatiliwa si na mtu mmoja. "Sijui ni nani ameweza kutambua au kutabiri kasoro hizo muda mfupi kama watu wanavyodai. Ninajua wapo watu wanaosema kuwa kwa kawaida chanjo huchukua muda mrefu kutengenezwa, ni sawa, nitafafanua," alisema.

Alisema ni kweli kutengeneza chanjo ya UVIKO-19 ilichukua muda mfupi huchukua hadi miaka10 hadi 20 na kinachofanya ichukue muda huo ni mifumo ya utengenezaji wa chanjo yenyewe.

"Lakini katika kesi hii ya UVIKO-19, Shirika la Afya Duniani (WHO) na kamati zote zinazohusika, walifanyia kazi chanjo hiyo kwa muda mfupi ili kukabiliana na dharura," alisema na kuongeza; "Sababu nyingine kwa nini chanjo hiyo ilipatikana haraka sana ni kwamba kulikuwa na majaribio ya chanjo kama hiyo kabla ya 2019."

Prof. Janabi alisema chanjo zinafanya kazi vizuri na kwamba kuna wakati alihisi dalili za mafua na alipochanjwa aliondokana na hali hiyo na sasa anaendelea kufanya kazi kama kawaida.

"Wapo wanaohoji faida ya kuchanjwa kwa kuwa bado wanaweza kuugua ugonjwa huo. Ni kweli bado unaweza kupata UVIKO-19. Tofauti ni kwamba aliyechanjwa hatapata mafua, na hata akipata hatalazwa hospitalini na atalindwa dhidi ya kifo," alisema.

Aidha, alisema wapo baadhi ya madaktari na wauguzi ambao badi hawajachanjwa na kufafanua kuwa wote ni wanadamu kama wengine na kwamba ugonjwa huo ni mpya, hivyo kila mtu, awe daktari au raia wa kawaida, mhandisi au mwanasheria wote wana hofu.

"Pamoja na hayo, suala la muhimu la kutambua ni kwamba nchi ina uwezo wa kudhibiti kila kinachoingia nchini zikiwamo chanjo kwa kuhakikisha zinaletwa zile ambazo ni salama," alisema.

Alisema, kwenye taasisi anayoiongoza, wamechanja viongozi wengi wa umma na kwamba wapo wengi wanaokwenda kwa ajili ya dozi ya pili.

Prof. Janabi alisema ugonjwa huo una athari kubwa, na kwamba wapo wagonjwa walipoteza pafu moja kwa sababu ya matatizo ya UVIKO-19, wengine kupoteza uwezo wa kunusa harufu na hawawezi tena kunusa.

"Ndio maana ninashauri sana watu waende kuchanja ili kuepuka matatizo kama haya, lakini pia ninashauri kuwapo kwa elimu zaidi kuhusu ugonjwa huo madhara yake ili jamii ipate taarifa sahihi na kuchukua uamuzi wa kuchanjwa," alisema.

Alifafanua kuwa Wizara ya Afya kupitia kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma kwa kushirikiana na UNICEF na Taasisi ya Benjamin Mkapa wana jukwaa linalotoa taarifa sahihi kuhusu UVIKO-19, na kuwataka Watanzania kutumia jukwaa hilo ili kupata taarifa sahihi kuhusu ugonjwa huo.




Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza Autism Foundation, Hilda Nkabe, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mbio za marathoni kwa ajili ya kuwachangia na kuwaletea matumaini watoto wenye uhitaji. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Amwombea msaada mwanawe matibabu ya saratani ya macho



**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAMKE Agatha Bulunja (30) mkazi wa Ndala Manispaa ya Shinyanga, anaomba msaada wa matibabu ya mtoto wake, Jenety Betho (4), ambaye anakabiliwa na tatizo la saratani ya macho na haoni tena.

Aliomba msaada huo jana wakati akizungumza na Nipashe na kueleza, kuwa mtoto wake huyo hali yake inazidi kuwa mbaya na hana fedha za kumpatia matibabu ya kufanyiwa upasuaji.

Alisema alimzaa mtoto huyo mwaka 2018 akiwa mzima na macho yake yote yanaona, lakini alivyofikisha miezi saba ndipo tatizo la kuugua saratani ya macho likaanza.

"Mtoto huyu nilianza kumpatia matibabu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, na baadaye tukapewa rufani ya kwenda Muhimbili ndipo nikaambiwa anatakiwa afanyiwe upasuaji, lakini kutokana na kutokuwa na uwezo ikabidi nirudi nyumbani,"alisema Bulunja.

Aidha, alisema Januari mwaka huu hali ya mtoto huyo ndipo ikabadilika na kuwa mbaya zaidi, pamoja na kuota nyama kwenye macho na kuyaziba na kuacha kuona kabisa, huku akilia usiku kucha kwa kuugulia maumivu na kumpatia dawa za kutuliza maumivu hayo.

Alisema kutokana na hali ya mtoto wake kuendelea kuwa mbaya zaidi, anawaomba wasamaria wema wamsaidie ili mtoto wake apate matibabu na kurudi katika hali yake kama zamani.

Kwa upande wake mama mwenye nyumba ambayo amepanga mwanamke huyo, Efania Kelvin, alisema wamekuwa wakimpatia msaada wa mahitaji muhimu ikiwamo chakula, sababu hana kazi ya kumwingizia kipato kutokana na kubaki kumuuguza mwanawe hapo nyumbani bila ya mafanikio.

Alisema kutokana na hatua ya saratani ambayo amefikia mtoto huyo, ana hitaji kupatiwa matibabu katika hospitali kubwa, na kutoa wito kwa wadau ambao wataguswa na mtoto huyo wamsaidie ili apate matibabu.

Kwa mtu yoyote atakae guswa na habari na kuamua kumsaidia mwanamke huyo awasiliane naye kwa simu namba **0758267338**.

# TRA yawashauri w/biashara kuajiri wahasibu wenye sifa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kikodi wa Kahama mkoani Shinyanga, imewataka wafanyabiashara kuajiri wahasibu wazuri wenye sifa watakaowasaidia kufanya vizuri katika manunuzi ya bidhaa zao.

Wafanyabiashara wengi hawapo makini wanapokuwa wakifanya manunuzi yao kutokana na kusahau namba zao za utambulisho (TIN) mara kwa mara, hivyo kuwa tatizo wakati wa kufunga hesabu zao.

Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka hiyo, Elibariki Sanga, alitoa ushauri huo katika mafunzo ya wafanyabiashara na washauri wa biashara zao iliyofanyika mjini hapa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutuma taarifa zao (Ritani) kwa njia ya mtandao.

Sanga alisema, kutokuwa na wahasibu wa ndani kwa wafanyabiashara hao wenye sifa, kumekuwa na kikwazi kikubwa katika biashara, huku akiwasisitiza kuwa katika manunuzi ambayo wanakuwa wakifanya kila siku wakumbuke kuwa na namba zao za TIN.

Aidha alisema katika mafunzo hayo ambayo yalikuwa yakiwatoa katika mfumo wa zamani wa kutuma taarifa za (Efaill) na kuwaingiza katika mfumo mpya wa mtandano pia utawasaidia kufuata sheria za kodi wanapokuwa katika biashara zao bila kusumbuana na maofisa wa TRA.


Sanga ambaye alikiwa mwezeshaji katika mafunzo hayo, pia aliwataka wafanyabiashara hao kuacha tabia ya kutuma wawakilishi katika mafunzo kwani mafunzo ni muhimu kwa wamiliki pamoja na wale washauri wa mambo ya kodi wanaowatumia.

Meneja Ukaguzi kutoka TRA Mkoa wa Kikodi wa Kahama, Irene Hance, alisema mamlaka hiyo inaendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wake juu ya mabadiliko ya sheria na mifumo ya ukusanyaji wa kodi za serikali ili kuondoa changamoto zinazowakabili wakati wa utendaji.

Alisema mafunzo hayo ya uwasilishaji wa Ritani kwa njia ya mtandao ni muhimu kwa sasa na yatawasaidia wafanyabiashara katika mambo mbalimbali ya kodi kwani watakuwa wakizijaza taarifa zao bila ya kufika katika ofisi za mamlaka husika.

Aliongeza kuwa pia mafunzo hayo yatawasaidia kuwaondolea changamoto za kitaarifa kabla ya kufanya ukaguzi kwani atakuwa na uwezo wa kufanya masahihisho kabla ya kuwasilisha Ritani zake za makadirio ya kodi.

Hance alisema mpango huo wa kutuma taarifa kwa njia ya mtandao pia utasaidia kuepuka udanganyifu wa kudai risiti zaidi ya mara mbili kwa kutumia teknolojia hiyo ya mtandao pamoja na kudhibiti mianya mbalimbali ya ukwepaji wa kodi.



Mtaalamu wa mifumo ya kompyuta wa kampuni ya Vodacom Tanzania PLC, Omar Amir, akitoa maelezo kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Rumuli mkoani Kagera namna ya kutumia huduma ya E- Fahamu inayowezesha wanafunzi kupata elimu kidijitali mahali popote walipo, mafunzo hayo yaliandaliwa na Asasi ya Vodacom Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi wanolewa

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

KIKAO kazi na mafunzo kwa wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya wilaya nchini kimeanza jana mkoani Tanga.

Kikao hicho kinatarajiwa kuzinduliwa rasmi leo na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete.

Katika kikao hicho pamoja na uwasilishwaji mada, wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya nchini watapata mafunzo ya namna bora ya kuendesha mashauri ya ardhi pamoja na uandishi mzuri wa hukumu.

Katika siku ya kwanza ya kikao hicho Jaji wa Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi, Benhaji Masoud, aliwasilisha mada kuhusiana na masuala mtambuka katika uendeshaji mashauri ya ardhi.

Kikao hicho cha siku nne kinatarajiwa kumalizika keshokutwa.

**Katika kikao hicho pamoja na uwasilishwaji mada, wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya nchini watapata mafunzo ya namna bora ya kuendesha mashauri ya ardhi pamoja na uandishi mzuri wa hukumu.**

# Wasimulia ruzuku ya TASAF ilivyowakomboa

**Na Neema Hussein,** KIGOMA

MPANGO wa kunusuru kaya za maskini walengwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umetajwa kuwa mkombozi kwa kaya zilizokuwa zikiishi katika hali duni.

Kwamba ukombozi huo umekuja baada ya kuingia katika mpango huo na kuwezeshwa kwa kupewa fedha.

Uhawilishwaji huo unaofanywa na TASAF kwa kuwapatia kiasi cha fedha kwa kaya za walengwa umesaidia kaya hizo kuondokana na umaskini waliokuwa nao na kubadili maisha yao.

Walengwa wa kaya maskini zilizohawilishiwa fedha na mpango huo katika vijiji vya Kumbanga na Kumhasha vilivyoko Kata ya Mlungu Halmashauri ya Wilaya Kibondo mkoani Kigoma wamebainisha kuwa maisha yao yamebadilika.

Miongoni mwa walengwa walionufaika na mpango huo wa kunusuru kaya za walengwa ni kijana Shukuru Aloyce anayeshuhudia mafanikio aliyo nayo kutokana na mpango huo.

Shukuru alisema wazazi wake walikuwa miongoni mwa wanufaika wa mpango, na baada ya wazazi wote wawili kufariki aliteuliwa kuendelea kupokea ruzuku hiyo ambayo aliitumia kulea wadogo zake kwa kuwa yeye ndiye mkubwa na msimamizi wa kaya.

"Nilikuwa nikipokea fedha kutoka TASAF kidogo nilizitumia kwa matumizi ya nyumbani na wadogo zangu mwaka jana, TASAF walikuja na mpango wa kusaidia vijana waliokwama kuendelea na masomo," alisema Shukuru.

Alisema baada ya kupatiwa mafunzo ya siku saba walipewa fedha 170,000 na alianzisha biashara ya kuuza maandazi na vyombo vya nyumbani vilivyokuwa na mtaji wa Sh.80,000.

"Shilingi 90,000 nilinunua migomba na kuipanda kwa ajili ya biashara na matumizi ya nyumbani, faida niliyopata katika biashara ya umachinga nimenunua tripu moja ya mawe natarajia kujenga nyumba." alisema Shukuru.

Aliishukuru TASAF kwa kubadilisha maisha yake na familia yake kutoka hali duni aliyokuwa nayo hadi sasa angalau ana unafuu wa maisha na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii.

"Naumia sana ninaposikia neno maskini, hivyo kupitia ruzuku hii ninayopokea kutoka TASAF nina imani nitaitumia vizuri mpaka niondokane na umaskini," alieleza Shukuru.

Naye mzee William Selele alisema ruzuku waliyokuwa wakiipata yeye pamoja na mke wake waliitumia pia kusomesha watoto wao shule na anaamini watakapomaliza watakuwa msaada katika maisha yao.

Mtendaji wa Kijiji cha Kumbanga, Zabron Bangaya, aliupongeza mpango wa kunusuru kaya maskini kutoka TASAF na kusema awali hali ya umaskini ilikuwa ya kutisha katika Kkijiji hicho, lakini baada ya kaya maskini kuanza kupokea ruzuku kutoka TASAF hali imebadilika katika kaya hizo.

Bangaya alisema pia kuwa watoto wanaosomeshwa na wazazi walioko katika mpango wa kunusuru kaya maskini wanapohitimu masomo yao na kupata kazi wasitelekeze kaya zao hasa wazazi waliowasomesha.

Ukurasa 12


Jinamizi watoto kukimbia shule kuhamia ajira inavyotesa wazazi

Ukurasa 13


MIAKA 100 YA MWALIMU NYERERE

Aliwekeza katika elimu wakati wote 'ikajibu' ngazi kimataifa

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 5, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

TEA na mfuko elimu SDL unavyowapa tija maskini

ELIMU

NA THOBIAS MWANAKATWE, BABATI

# Wadau binafsi wanavyopenya kufikisha elimu wafugaji waliko

• Ole Toima; DC mstaafu katika ajenda mpya

KUNA jitihada mbalimbali zinafanyika kuinua sekta ya elimu nchini, serikali ikishirikiana na sekta binafsi, huku uhusiano ukichukua sura katika mfumo wa ubia wa sekta binafsi na umma.

Hata hivyo, jitihada za kuinua elimu hususani katika maeneo ya wafugaji nchini, zimekuwa zikikumbana na changamoto nyingi, ikiwamo mila na desturi potofu, miundombinu, sanjari na mazingira yasiyoridhisha katika baadhi ya maeneo hayo.

Jumuiya ya wafugaji, ni miongoni mwa maeneo yanayohitaji msisitizo mkubwa kwenye uwekezaji. Elimu ni miongoni mwa maeneo yanayohitaji kutiliwa mkazo na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Hapo ndipo inakuja nafasi ya shirika lisilo la kiserikali la maendeleo la Eclat Development Foundation na wadau wengine, kuinua sekta ya elimu hususani maeneo ya wafugaji, bado yanahitaji msukumo mkubwa katika kupambana na kutokomeza ujinga nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Peter Ole Toima, anasema tangu kuanzishwa mwaka 2016, limeshawafikia na kuwagusa wanafunzi zaidi ya 17,000 nchi nzima, ni mafanikio makubwa.

Ole Toima, ambaye ni mkuu wa wilaya mstaafu, anataja baadhi ya maeneo taasisi yao imefanikiwa kuyafikia ni pamoja na wilaya za Simanjiro, Monduli, Kiteto Kilolo, Ruangwa, Tandahimba, Karatu na Ngorongoro.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Maendeleo la Eclat Development Foundation, Peter Ole Toima, akiwa ofisini. Mbele yake ni tuzo iliyotunukiwa asasi yake kwa ajili ya kufanikisha elimu. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

Anafafanua katika miradi ya elimu imefanikiwa kujenga shule 216 za msingi, sekondari 20, nyumba za walimu 14 , chuo kimoja cha ufundi stadi (Veta) mkoani Manyara.

Mkurugenzi huyo anajisifu shirika lao limefanikiwa kujenga shule katika maeneo yasiyofikika kirahisi, hususani maeneo ya wafugaji ambayo mwamko wa elimu bado upo chini.

Anaeleza, pia wamekarabati shule zenye miundombinu chakavu, vyoo vya shule, madarasa, nyumba za walimu, ofisi za walimu sanjari na kuweka samani ndani ya shule hizo.

Ole Toima anasema, shirika lao limejikita katika miradi ya afya na maji, pamoja na kuanzisha programu maalumu za kuwainua wanawake nchini.

Anasema lengo la miradi hiyo, ni kuwafikishia elimu wananchi wa maeneo ya kifugaji ambao wamekuwa hawafikiwi kirahisi jambo ambalo wamefanikiwa kutekeleza kwa kujenga takribani vyumba 260 vya madarasa.

"Tumefanikiwa kujenga kituo cha wanawake kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi, tumefanikiwa kuanzisha vikundi zaidi ya 70 vya wanawake ili waondokane na hali ya kuwa tegemezi," anasema Ole Toima.

Anasema kwamba katika programu hiyo walianzisha idara ya wanawake ambapo malengo yake ni kuwapatia elimu ya afya, ujasiriamali, uzazi wa mpango na kuwapatia mitaji ya biashara.

"Tuna utaratibu wa kuviwezesha vikundi hivi, tunawapatia mitaji kuanzia shilingi milioni mbili na wanarejesha kuanzia asilimia 20 kwa awamu tatu, hiyo pesa wanayorejesha inaenda kwa vikundi vingine," anafafanua.

Ole Toima anasema kwamba shirika lao limejiwekea malengo ya kuondoa ujinga katika jamii ya Watanzania hususani wa kutojua kusoma na kuandika.

Ole Toima anasisitiza: "Tukitaka mabadiliko ya kweli ni lazima tuwekeze kwenye elimu jamii zetu lazima zibadilike na elimu ina uwezo wa kumbadilisha mtu," anaeleza Ole Toima.

**CHANGAMOTO**

Mkurugenzi huyo anaeleza changamoto zao, ni pamoja kulinganisha na uwezo wao, akifanua shirika lao linategemea kwa asilimia kubwa ufadhili kutoka kwa wahisani nje ya nchi na hivyo kuna muda wanalazimika kusubiri fedha za wahisani ili watekeleze majukumu yao.

Anataja changamoto nyingine, inahusu miundombinu hata wanalazimika kutekeleza baadhi ya miradi nyakati za kiangazi badala ya masika, kwa kuwa maeneo mengi hayafikiki nyakati za masika, kutokana na uharibifu wa miundombinu.

Ole Toima, anaeleza zaidi ya Sh. bilioni 12 zimetumika kugharamia miradi mbalimbali katika mikoa tisa na wilaya sita nchini katika kipindi cha miaka sita tangu kuanzishwa kwa taasisi yao.

Anakiri ushirikiano baina yao na serikali ni wa kuridhisha, kwa kuwa wamekuwa wakishirikiana na kamati za shule, wahandisi wa halmashauri pamoja na wataalamu mbalimbali serikalini ambao wamekuwa na msaada mkubwa katika majukumu yao.

ELIMU

NA RAHMA
SULEIMAN, PEMBA

SHIDA YA TAALUMA...

# Jinamizi watoto kukimbia shule kuhamia ajira inavyotesa wazazi

NI Jumanne saa 3:30 asubuhi katika ufukwe wa bahari ya kijiji cha Kiuyu, wilayani Micheweni, Pemba, muda wa wavuvi kurudi baharini baada ya usiku kuchwa wa kutafuta riziki.

Kwa kawaida muda huo watoto wanatakiwa kuwa shule wakiendelea na masomo, lakini hali ni tofauti kijijini hapo. Nipashe inawakuta watoto wakiwa na visu wamekusanyika na wanajiandaa kupaa samaki wanaonunuliwa na wateja kama sehemu yao ya kujipatia kipato.

Ali (14) aliyekatisha masomo akiwa darasa la tano mwaka 2019, ni mmoja wa waliopo ufukweni wakiwasubiri wavuvi. Tangu aache shule, anasema amekuwa akifanya kazi hiyo ufukweni, kilichomsukuma akidai ni maisha magumu ya familia yake.

"Nilikuwa naenda shule na njaa, nyumbani hakuna chakula nalazimika kusubiri hadi usiku," anasema mtoto huyo.

Hata hivyo, anasema maisha yake yamebadilika kidogo baada ya kujiingiza katika ajira hiyo akipatiwa ujira wa Sh.5,000 kwa siku, licha hakupaswa kufanya kazi hizo wakati huu. Anasema ni fedha zinazomsaidia mama yake, ambaye ni mjane kukidhi mahitaji ya nyumbani.

Anasimulia alitamani awepo shule kama watoto wenzake, lakini hali ngumu ya maisha imemwingiza katika ajira akiwa mdogo kutafuta fedha kuisaidia familia.

Sheria ya Mtoto ya hapa, inakataza utumikishaji watoto, badala yake wanaruhusiwa kufanya kazi ambazo si za mateso na hazitawanyima haki kama za elimu na kusaidia baadhi ya huduma nyumbani, ikiweka bayana kumtumikisha mtoto kwa ajira ni kosa la jinai.

Zume Haji (12), aliyeacha shule darasa la nne, anasema aliingia kufanya kazi ya kupaa samaki kama ni sehemu ya kumwingizia kipato.

Anasema, ameshawishika kuingia katika kazi hiyo baada ya kuwaona watoto wenzake wakifanya kazi hiyo, inayowapatia fedha na kununua vitu kama nguo za sikukuu.

"Nilipoona watoto wenzangu wanarudi nyumbani na pesa nikapata shauku na mimi kuongozana nao, kuanzia hapo nilisalia hapa na sikurudi tena shule," anasema.



Baadhi ya watoto wakipaa samaki katika Pwani ya Unguja Ukuu Mkoa wa Kaskazini Unguja eneo ambalo ni maarufu kwa mnada wa samaki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

> Nilipoona watoto wenzangu wanarudi nyumbani na pesa nikapata shauku na mimi kuongozana nao, kuanzia hapo nilisalia hapa na sikurudi tena shule.

### UKUBWA WA TATIZO

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, inataja watoto 7,609 katika wilaya ya Micheweni wapo nje ya mfumo wa elimu sawa na asilimia 21.7.

Hata hivyo, inataka kati wapo 11,000 wamerejeshwa shuleni. Inaelezwa wameacha shule kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kujiingiza katika ajira za utotoni kama uvuvi, kubanjua kokoto, kuchonga matofali na biashara ndogo.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Kiuyu Mbuyuni, Suleiman Daudi Mkasha, anasema tatizo la utoro kwa wanafunzi huwa kubwa zaidi wakati wa 'bamvua' (msimu mkubwa wa samaki).

Katika Shule ya Msingi Kiuyu Mbuyuni, wastani wa wanafunzi 120 kwa siku wanatoroka shule, kwenda katika shughuli zinazohusiana na uvuvi.

Katika shule jirani Micheweni, wastani wa watoto 10 hadi 15 katika darasa moja lenye wastani wa wanafunzi 90 wanatoroka shule, wengi wao ni wavulana.

"Utoro huu upo zaidi kwa wanafunzi kuanzia darasa la nne hadi la sita wengi hukimbilia baharini kupara samaki kwa watoto wavulana na wasichana ukulima wa mwani," anasema Mwalimu Mkuu.

Anasema ukosefu wa elimu ndio chanzo cha wazazi kuwaruhusu watoto kujiingiza katika ajira hizo ambazo zinawanyima haki ya kupata elimu, pia wazazi wenyewe ndio wanaowashawishi watoto kufanya kazi hizo, kwa lengo la kupata fedha bila ya kujali umuhimu wa elimu kwa watoto wao.

Anataja katika shule hiyo yenye wanafunzi 1060 ambapo 70 wamerejeshwa shule kati ya hao wavulana 26 na wasichana 43.

Kwa mujibu ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, kiwango cha wanaojua kusoma na kuandika katika wilaya ya Micheweni ni asilimia 40 kwa wenye umri wa miaka mitano na kuendelea.

Waliojua kusoma na kuandika kwa Kiswahili walikuwa asilimia 30, huku asilimia 19 wakiwa wanajua kusoma na kuandika kwa Kiingereza.

Ni kiwango kinachochangiwa na wanafunzi kuacha shule katika umri mdogo au wengine kutoandikishwa kabisa shule.

Mwaka Hamad mkazi wa Kijiji cha Kiuyu Mbuyuni, anakiri watoto wamejiingiza katika ajira na kukatisha shule kwa sababu familia zinashindwa kutimiza mahitaji yao.

"Watoto wanakosa sare za shule, madaftari na wakirudi nyumbani hakuna chakula... je katika mazingira kama haya mtoto kweli atasoma," alisema.

### MAONI YA WADAU

Kombo Massoud, ni mnunuzi wa samaki katika bandari ya Kiuyu Mbuyuni. Anafika hapa kila Jumapili kwa ajili ya kununua samaki kwa matumizi ya nyumbani.

Anasema anatambua kwamba kuwatumikisha watoto ni kinyume cha sheria, lakini anachofanya ni kuwasaidia kupata fedha za kujikimu kutokana na hali ngumu ya umaskini," anafafanua.

Mchuuzi wa pweza, Time Khamis, anasema baada ya kununua kitoweo hicho huwapa watoto kuwagonga ili walainike, hata hivyo, anajitetea haelewi kama anachofanya ni kuwatumikisha watoto. Bala anaamini ni sehemu ya kutafuta riziki zao.

Dk. Mwatima Juma, Mkurugenzi wa Jumuiya ya Kuwaendeleza Wasichana Kielemu Afrika (FAWE), Ofisi ya Zanzibar, anasema wawasaidia watoto kutoka familia maskini hasa wasichana ili kuhakikisha wanapata elimu.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa anasema lazima kuwapo ufuatiliaji wa watoto waliotoroka shule na kujiingiza katika ajira.

Lingine anataja, haja ya kuwepo usimamizi wa sheria za kuwalinda watoto na wale wote wanaowatumikisha kupewa adhabu kali ili kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia hiyo.

### MKAKATI SERIKALINI

Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, Zuhura Mgeni, anasema baada ya kugundua watoto wengi wapo nje ya mfumo wa elimu na kujiingiza katika ajira za utotoni, serikali imeanza kuchukua hatua za kuwarejesha shuleni.

ELIMU
NA PETER
ORWA

MIAKA 100 YA MWALIMU NYERERE

# Aliwekeza katika elimu wakati wote 'ikajibu' ngazi ya kimataifa

• Elimu Kujitegemea, alama ya kudumu

SHAMRASHAMRA za kuadhimisha miaka 100 tangu kuzaliwa kwa Hayati Mwalimu Julius Nyerere zinaendelea.

Iwapo mtu anaulizwa swali, ni kipi kilikuwa kipaumbele chake kisera? Ni kwamba serikali ya awamu ya kwanza, tangu kupatikana uhuru hadi anaondoka madarakani, ni chanda na pete kwa elimu.


Na inapoangaliwa kwa kina, Mwalimu Nyerere, ambaye ajira yake pekee uraiani ilikuwa 'kushika chaki' daima kwa matendo hajawahi kuiacha fani hiyo, maana amekuwa mtu wa maelekezo na mafunzo kila awapo.

Mfano hai ni pale anapohutubia akifafanua namna ulimaji mpunga unapandwa na kuota kwa ufanisi kwa umbali wa nchi moja.

Pia ameandika vitabu vingi, kutaja vichache ni Ujamaa; Binadamu na Maendeleo, huku akitoa nadharia ya elimu nchini; Elimu ya Kujitegemea. Ni nadharia, ambayo inadumu katika Sera ya Elimu nchini hadi sasa, ikabeba maana hata katika mazingira ya sasa.

Ni baada ya uhuru mwaka 1961, aliutwaa uongozi wa nchi taifa likiwa na pengo kubwa la fursa ya elimu katika sura kuu tatu; ikitolewa kitabaka, Wazungu wakiwa na fursa zaidi, kufuatia Waasia na Waafrika walipata nafasi kidogo, pia wakiishia ngazi za chini.

Mwaka huo 1961, Mwalimu Nyerere alichukua hatua kuu tatu; ambazo zote zilikuwa katika mpango wa kwanza wa miaka mitatu, 1961 hadi 1964. Nafasi ya elimu shuleni kuwa kwa wote, bure na kutanuliwa bajeti ya taifa katika elimu, jambo ambalo hajawahi kulibadili.



Mwalimu Nyerere, alipokutana na Rais John F. Kenedy wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

### BAADA YA 1964

Mwaka 1964 ambao ndio sehemu ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo nchini ulianza, pia ilijikita zaidi katika elimu na hasa ya msingi. Hapo kukawapo utanuzi wa elimu kufikia ngazi ya kila kijiji kitaifa.

Ulipofika mwaka 1967, Mwalimu Nyerere kupitia chama - TANU, alipotangaza Azimio la Arusha, katika tafsiri yake 'Njia pekee nchi itakavyotaliwa kupitia Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.'

Hapo, Mwalimu Nyerere katika hatua hiyo ya mwaka 1967 akazindua maandiko ikiwamo kitabu cha 'Ujamaa Essays'. Hiyo ikaenda sambamba na kubuni mwongozo wa elimu kitaifa; ambayo ina jina Elimu ya Kujitegemea.

> Hadi kufika 1975, Tanzania, iliweka rekodi kubwa kitaifa kuwa na sehemu kubwa ya raia wake wanaojua kusoma na kuandika, pia watoto kwenda shule.

Kwa mujibu wa mwongozo huo ambao umebeba sura ya nadharia, unataja maudhui ya elimu nchini ina sura ifuatayo: Kila ngazi ya elimu iwe inajitegemea; ikimaanisha mathalan mtu anaposhindwa kufika darasa la saba, elimu imsaidie kuwajibika katika maisha yake na si kutamka 'amefeli kuendelea.'

Pili, inataka aina ya elimu itolewayo nchini, maudhui yake na mitaala, ifanane na uhalisia wa maisha yake na si vinginevyo. Hapo ndipo kukashuhudiwa masomo kama Elimu ya Siasa wakati huo, huku sekondari kukiwapo mikondo ya kilimo, biashara na ufundi.

Pia ni wakati ulipopigwa marufuku shuleni wimbo wa wanafunzi hasa madarasa ya chini "London is burning hurry up, hurry up!...' na kubakishiwa mirindimo ileile kwa mashairi "...Eeeh Yakobo amka twende shule...haya njoo" ili iwe ya Kitanzania zaidi.

Tatu, akahimiza ekimu ya Kitanazania isiegemewe katika mtazamo wa ajira ya ofisini pekee, bali ijielekeze nje ya ofisi.

Nne, katika nadharia hiyo inamtaka msomi wa Kitanzania kwa ngazi yoyote ile, daima abaki kuwa sehemu ya jamii yake katika maisha yake ya kawaida na elimu aliyoipata kuwa msaada kwa uma ambao umekosa fursa ya elimu.

Ndio maana hata wakati huo, serikali ilisema waliovuka darasa la saba kwa kuwa walikuwa wachache waliambiwa 'wamechaguliwa' na si kufaulu.

Hiyo inashuhudiwa hata ilipowekwa miradi ya elimu kwa watu wazima na umma kuiendeleza, kulikuwapo na walimu wengi wa kujitolea.

Wakati huo kiasi kikubwa shule za sekondari ni zile kongwe zilizorithiwa kutoka zama za ukoloni.

### MAGEUZI YA 1974

Ni wakati wenye tafsiri pana katika elimu kitaifa, ikianzia na kupitishwa Azimio la Iringa lililotilia mkazo katika elimu, ikiwa ni mwendelezo wa kilichoamuliwa kati ya mwaka 1964 na Azimio la Arusha 1967.

Ni mwaka ambao kulikuwapo operesheni kuundwa vijiji vya Ujamaa, ambavyo ujenzi wake pia uliangukia kuhakikisha kuna huduma zote muhimu, ikiwapo shule ya msingi.

Pia, mwaka mmoja kabla ya 1974 ndio kukaundwa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na mwaka 1976 kukaundwa silabasi mpya ambayo ilikuwa na maudhui yenye sura kamili ya Kitanzania.

Hadi kufika 1975, Tanzania, iliweka rekodi kubwa kitaifa kuwa na sehemu kubwa ya raia wake wanaojua kusoma na kuandika, pia watoto kwenda shule.

Katiika kipindi chote kwa utawala wa Mwalimu Nyerere, bajeti ya sekta ya elimu ilikuwa juu hasa na hata kufikia miaka ya 1970 iligusa hadi asimilia 25 ya bajeti yote.

Hiyo iliendana na kasi ya kujengwa vyuo vya ualimu nchini kwa wingi, mfano hai Chang'ombe ambacho sasa kinajulikana kama DUCE, chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaaam.

Pia maofisa elimu kata vijijini, kama walivyo maofisa ugani kilimo waliokumbushwa enzi zao jana na zawadi kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, walipewa pikipiki Honda Trail, kuwarahisishia kazi zao.

### ELIMU WATU WAZIMA

Mapema tu baada ya Uhuru Rais Nyerere, kutumia uelewa wake na kiutawala na fani ya ualimu, akijua kulikuwa na kundi kubwa la Watanzania waliokosa fursa kuanzia ngazi ya juu na wasiojua kusoma na kuandika, aliunda Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Taasisi hiyo iliratibu jukumu hilo kwa mafanikio makubwa, Watanzania wengi wakajua kusoma na kuandika na wapo waliosonga kwenda ngazi ya sekondari na zaidi.

Hiyo kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa, ikiwamo za Umoja wa Umoja kulianzishwa Mpango wa Elimu kwa Wote (UPE), ambao nao umechangia sana na kukomboa umma.

Katika upanuzi huo, kuna wakati ukafanyika mpango wa wahitimu wa darasa la saba, kupigwa 'brashi' wakawa walimu, tena kwa mafanikio ambao wamechangia sana rekodi ya Tanzania kung'ara Afrika katika elimu mwaka 1975.

Wakati Mwalimu Nyerere anaweka juhudi hizo mwanzoni mwa mwaka 1970, Jumuiya ya Waislamu Tanzania (BAKWATA) ikatoa mchango wake kupanua sekondari, shule binafsi kama Jumuiya (Tanga) na Kinondoni, Dar es Salaam.

Ikifuatiwa mwaka 1976, Jumuiya ya Wazazi Tanzania nayo ikafuata. Hapo kuna shule kama Vituka, Lupata, Ovada, Boza na Bagamoyo zote za mkondo wa ufundi.

ELIMU
NA JOSEPH MWENDAPOLE

# TEA na mfuko elimu SDL unavyowapa tija maskini

MFUKO wa Kuendeleza Ujuzi (SDL) ulioko chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na unatekelezwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), hadi sasa una miaka mitano ukiwa umeshapiga hatua kubwa kwa kuwapa ujuzi unaowezesha kujiajiri na kuajiri.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, anasema mfuko ulianzishwa kuwaendeleza vijana wajiajiri baada ya kuhitimu masomo yao na unatarajia kuwanufaisha vijana 38,000 itakapofika mwezi Juni mwaka huu.

Geuzyei anakitambulisha ni chombo kilichoanzishwa mwaka 2017, kikiajiri vijana 31,984 waliokwisha nufaika na mafunzo ya kuendeleza ujuzi kwenye ufugaji, kilimo, utengenezaji batiki, ufundi stadi yanayotolewa na mfuko huo.

Anasema, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa mafunzo yaliyojikita katika sekta za Kilimo na Kilimo Biashara, Sh. bilioni 3.1 zilitengwa kuzinufaisha taasisi 15.

Anasema awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi ulianza katika mwaka wa fedha 2019/20 na 2020/21 kwa Sh. Bilioni 9.7 kunufaisha taasisi 81 za mafunzo kuwezesha wanufaika kwa kupata ujuzi katika sekta sita zenye vipaumble ambazo ni; Kilimo na Uchumi, Utalii na Huduma za Ukarimu, Uchukuzi, Ujenzi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Nishati.

"Hadi kufikia Machi 2022, TEA imetoa Sh. bilioni 8.1 kwa miradi 81 ambayo wanufaika 30,590 ikiwa ni wanaume 15,634 na wanawake 14,956 wamepatiwa mafunzo," anasema.

Anasema Sh. milioni 385.778 zinatarajiwa kunufaisha vijana 1,018 katika sekta za teknolojia ya habari na mawasiliano, utalii na huduma za ukarimu, nishati, ujenzi na uchukuzi

"Mfuko wa SDF pia unafadhili mafunzo kwa wanufaika 4,000 kutoka kaya maskini na makundi maalum hadi ifikapo Juni 2022. Hadi Agosti 2021, jumla ya wanufaika 1,627 walipata mafunzo katika awamu ya kwanza ya mpango huu," anafafanua.

Pia anaitaja awamu ya pili ya ufadhili ulioanza mwezi huu, kunatarajiwa wanufaika 2,373 wanatapatiwa mafunzo kabla ya mwezi Juni 2022.

**MIRADI YA ELIMU**

TEA, inaendelea ufadhili miradi mbalimbali ya elimu na mpaka sasa jumla yao ni 3,314 yenye thamani ya Sh. bil. 212.6 tangu kuanzishwa mwaka 2001.

Mkurugenzi Geuzye, anasema ruzuku ya Sh. bilioni 200 zilitolewa, ikiendana na mkopo nafuu wa Sh. bilioni 12 kwa shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, ufundi na vyuo vikuu. Anasema, ni hali inayoibua ujenzi wa mabweni 73, vyumba vya madarasa 1,050, matundu ya vyoo 5,880 na nyumba za walimu 560 katika shule 791 za msingi na sekondari.

Mkurugenzi anafafanua, TEA imeratibu ukarabati wa shule 17 za sekondari kongwe, ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa kwa shule 71 za msingi na sekondari, zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Anatahja lingine ni mafunzo maalumu ya kuongeza uwezo wa kitaaluma wa wanafunzi 2,196 wa kike, TEA ikiandaa na kuchapisha muhtasari, mitaala na vitabu vya kiada kuanzia darasa la tayu hadi la sita.

Anaitaja miradi mingine iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa kwa vyuo vikuu akivitaja: Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius K. Nyerere, (MJNUAT), Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume (KIST), Taasisi ya Utawala wa Umma (IPA) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mkurugenzi Geuzye, anasema katika mwaka wa fedha 2014/15 na 2015/2016, TEA ilifadhili mafunzo ya kujenga uwezo katika Programu ya Matokeo Makubwa, ikifadhili mafunzo ya kujenga uwezo kwa wakufunzi na walimu wa shule za msingi wa masomo ya Kiswahili, Hisabati na Kiingereza.

Anasema, wameshatoa mafunzo kwa walimu 6,000 wa shule za sekondari wa masomo ya Baiolojia, Kiswahili, Hisabati na Kiingereza na kuliwezesha Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) kupanga matokeo ya ufaulu na kuchapa vitabu vya maswali ya mitihani.

## WANENAVYO MALENGA

### Msukule kaamka

Tusiwe wadanganyika, mwishowe tukapinduka,
Kuamini kwa haraka, mitume wa kujiweka,
Ambao wazukazuka, na yao yatamanika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Na kumbe zetu sadaka, ndio hasa wazitaka,
Wadhani watoa zaka, kumbe huko kunanuka,
Yazidi kueleweka, kwamba undanganyika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Vichwa vikichunguzika, hivi vinavyozunguka,
Akili zakamilika, au zimeshalipuka?
Mbona mengi yasikika, macho yameshapofuka?
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Hakuna anoshituka, kujidai wa Rabuka,
Uongo anaupika, aweze kuaminika,
Na watu wanaehuka, kwao anaaminika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Akili ndugu funguka, usiwe mdanganyika,
Upepo unapozuka, usije kupepesuka,
Hapo umejisimika, Neno zidi kulishika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Kibwetere wakumbuka, Uganda yalowafika?
Wengi walidanganyika, yake yakaaminika,
Nyuma aliwazunguka, wakafa wakafutika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Na haijafahamika, na yeye yalimfika,
Au moto alikoka, kawachoma katoroka,
Mamia walifutika, tukabaki kuwazika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Dini zinazoibuka, na mitume waibuka,
Zumu uwe na hakika, watumika kwa Rabuka,
Wengine yaaminika, na mwovu wanatumika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Mbinu nyingi zatumika, ili waweze kuteka,
Wakikuweka mateka, si rahisi kuchomoka,
Mapishi watakupika, hadi unamalizika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Bora ziende sadaka, mbele upate zinduka,
Usijekuwa mateka, jehanamu ukafika,
Usinziaye amka, usijekudanganyika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Neno la Mungu hakika, yake nayatimilika,
Alisema watafika, wale wa kunufaika,
Na wengi watawateka, hasara itawafika,
Msukule kaamka, ujumbe umetufika.

Yalosemwa yamefika, ni mengi yanasikika,
Huko nyasi zinalika, na hao waaminika,
Tena watu wafurika, miujiza kisikika,
Msukula kaamka, ujumbe umetufika.
**Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### Simu zisije nyumbani

Simuzi sije nyumbani, zibakie ofisini,
Watoto wako nyumbani, wakumbate mikononi,
Hata wakubwa nyumbani, sema nao sebuleni,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Watoto wako shuleni, na wewe uko kazini,
Au kazi za sokoni, posho yende mdomoni,
Inapofika jioni, nyote mwafika nyumbani,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Sasa watoka kazini, simu iko mkononi,
Wanakula kinyumbani, simu ikosikioni,
Wanakucheki usoni, wewe kama huwaoni,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Watoto pale nyumbani, wanahamu ya moyoni,
Wacheze kwako mwilini, waangalie usoni,
Wakija hawakuoni, simu iko akilini!
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Unaye mwenzi nyumbani, ndoa ya madhabahuni,
Ni kama haumuoni, tabasamu halioni,
Anakuona lakini, na simu u kichekoni,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Hamkuwepo nyumbani, hadi kufika jioni,
Simu zabaki mwilini, ni kama hamuonani,
Watoto wako shidani, na nyie mu matatani,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Iingie akilini, simu ziwe kifungoni,
Kama vile kanisani, ziwekwavyo mfukoni,
Au hospitalini, kwamba zisiwe mwilini,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Maisha yetu nyumbani, tunapokaa mezani,
Muda mzuri jamani, kusemezana kindani,
Siyo simu mkononi, kama tuko ugenini,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Na tukiwa sebuleni, tusiwe kama wageni,
Kama tunayo madeni, kwa kuinamia chini,
Kumbe huko mikononi, simu ziko akilini,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.

Tenga muda wa nyumbani, kuyafanya ya nyumbani,
Simu zikae pembeni, turidhishe wa nyumbani,
Tutazamane usoni, si maneno mdomoni,
Simu siyo mbadala, furaha ya familia.
**Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Uongozi wa soko washauriwa kuhusu ukusanyaji mapato

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA masoko wa Jiji la Dodoma, Steven Maufi, amewataka viongozi wa umoja wa wafanyabiashara wa soko kuu la Majengo jijini hapa waliochaguliwa kutokwamisha ukusanyaji wa mapato.

Maufi alisema hayo kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa umoja wa wafanyabiashara ulifanyika katika soko hilo.

Akizungumza na viongozi hao aliwataka kuhakikisha wanajenga umoja na mshikamano kati yao na Halmashauri ili kuhakikisha shughuli mbalimbali zinazofanyika hazikwamishwi kwa pande zote mbili.

Alisema kuwa ili maendeleo yaweze kuja kwenye soko hilo viongozi wanatakiwa kuwa kitu kimoja na wanaondokana na makundi ambayo yanayoweza kusababisha migomo isiyokuwa na tija kwa wafanyabiashara wenyewe na kwa halmashauri.

"Niombe nitoe rai kwenu nyinyi viongozi mliochanguliwa mhakikishe mnajiepusha na masuala ya migomo na kusababisha kukwamisha ulipaji wa ushuru na mkaleta hasara katika halmashauri pasipokuwa na sababu za msingi.

"Tunatakiwa kufanya kazi kwa umoja na kuwaweka wafanyabiashara kwa pamoja kwa kuwa wote ni sawa na tuwajibike kuwahudumia kwa usawa na ubora unaotakiwa," alisema.

Maufi aliutaka uongozi uliongia madarakani kufanya kazi kwa uwazi na kufanya mikutano ya kikatiba na kusoma taarifa ya mapato na matumizi ili kuondokana na migogoro.

Alisema katika uchaguzi huo uliofanyika umefanywa kwa demokrasia na kikatiba na wamepatikana viongozi ambao watahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu.

Aliufafanua kuwa jumla ya wanachama 1,455 walijiandikisha kupiga kura, lakini waliojitokeza kupiga kura walikuwa 850.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Majengo, Odilia Kota, alisema viongozi wa soko kuu la majengo wanatakiwa kuwa wachapa kazi na siyo wapigaji wa porojo.

# Chuo cha wapigania uhuru kukarabatiwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MABALOZI kutoka nchi za kusini mwa Afrika wameahidi kufanya ukarabati wa Chuo cha Mafunzo ya kijeshi ya wapigania Uhuru kutoka nchi zao, huku wakisisitiza kuendelea kutunza historia.

Wamebainisha hayo wakati wa ziara ya kutembelea Wilaya ya Kongwa kujionea kambi na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi ya wapigania uhuru kutoka nchi zao iliofanyika mwishoni mwa wiki.

Mabalozi hao ni wa Msumbiji nchini, Ricardo Mtumbuida, Balozi Sandro Renato Agostinho De Oliveira (Angola) na wengine ni kutoka Namibia, Zimbabwe na Afrika Kusini.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake Balozi Mtumbuida alisema lengo la ziara hiyo ni kujionea na kujifunza hali ya historia ya nchi zao na kushirikiana na serikali ya Tanzania kuangalia namna ya kuitunza.

"Tumekuja kuona makazi ya wapigania uhuru wa Msumbiji, Angola, Afrika Kusini, Namibia na Zimbabwe ili kuona jinsi yalivyo na tumeona yameanza kuharibika, tukirejea Dar es Salam tutakutana ili kufanya mipango ya kuisaidia wilaya na serikali ya Tanzania kufanya kazi kwa pamoja ya kukarabati ili historia isipotee," alisema Balozi Mtumbuida.

Kwa mujibu wa balozi huyo, nchi nyingi za Afrika zilipata msaada wa kujipatia uhuru wake kutoka Tanzania.

"Sisi tuliungwa mkono na Tanzania na tunamshukuru Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere kwa sababu aliweza kuwasukuma wenzake aliwahi kusema kuwa Tanzania haitakuwa huru kama nchi zote za Afrika hazijapata uhuru, ndio maana akatushika mkono tukafungua hili eneo," alisema. Naye Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remedius Mwema, alisema ni heshima kubwa wilaya hiyo kuwa miongoni mwa historia ya ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika.

Alisema ni vyema Watanzania wakathamini historia iliyoko Wilaya ya Kongwa kwasababu inahamasisha uzalendo, mahusiano mazuri yaliyojengwa na viongozi wa mataifa yote ya wapigania uhuru.

"Uwapo wa historia hii hapa Kongwa inatusaidia kuongeza uthamani na kutumia eneo hili kama sehemu ya mafunzo ambapo wanafunzi, na wageni kutoka maeneo mbalimbali wanakuja kutembelea, tunafanya eneo hili kuwa ni kichocheo cha uchumi kwa sababu wageni wakija wengi watahitaji kulala, kula hivyo itasaidia kuinua uchumi wa watu wa Kongwa," alisema Mwema.

Mwema alisema Kongwa ni sehemu muhimu inayokumbusha kazi zilizofanywa na viongozi wakubwa miaka ya nyuma.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, White Zuberi, alisema wilaya hiyo ina historia ndefu kutokana na kuwa na kambi ya ukombozi ya wapigania uhuru wa Afrika.

Kwa Mujibu wa Mwenyekiti huyo kambi hiyo ilijengwa mwaka 1964 ambapo wapigania uhuru kutoka nchi hizo walikuwa wakiishi kwenye kambi hiyo.



Maofisa wa Benki ya CRDB tawi la Ruangwa wakitoa elimu ya umuhimu wa Vitambulisho vya NIDA na utunzaji wa fedha kwa wanakijiji wa Nangurugai wilayani Ruangwa mkoani Lindi, hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usimamizi wa lishe kuendelea kuwa kipaumbele

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuratibu na kusimamia sera zinazohusu masuala ya lishe kama hatua ya kukabiliana na utapiamlo na udumavu katika jamii.

Mkurugenzi wa Idara ya Mipango na Bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu, Eleuter Kihwele, alitoa kauli hiyo kwenye semina ya kuwajengea uelewa menejimenti ya ofisi hiyo kuhusu utekelezaji wa mpango wa pili jumuishi wa masuala ya lishe iliyotolewa na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC).

Alisema kulingana na mpango wa taifa wa lishe wa miaka mitano umesisitiza ushirikishwaji wa sekta binafsi kushiriki katika hatua zote za kupanga na kutekeleza mipango inayohusiana na lishe pamoja na ushiriki wa wananchi wenyewe.

"Suala la lishe ni mtambuka linalohusisha wadau wote na wananchi hasa katika muktadha mzima wa kubadili tabia ya ulaji wa vyakula unaozingatia misingi ya lishe kuwa na nyaraka hizi za mpango wa miaka mitano ambazo zitakuwa ni rahisi kueleweka kwa wananchi na kutekeleza.

Pia ni lazima tuimarishe uratibu na ugharamiaji wa utekelezaji wa mpango ili yote yatekelezwe kikamilifu ifikapo 2025/2026," alisema.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ina jukumu la kuhakikisha shughuli za lishe nchini kwa kuzingatia kuwa kama nchi imeandaa mpango wa miaka mitano wa kuratibu masuala ya lishe baada ya kumalizika kwa mpango wa kwanza wa masuala hayo ambao umetekelezwa kwa miaka mitano.

"Mkutano huu umekuwa na manufaa makubwa kwa washiriki na wadau waliohudhuria kufahamu ni wadau gani wanaopasawa kusimamia masuala haya hivyo imekuwa ni fursa muhimu kwa menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana ya uongozi na wakuu wa idara ambao wanasamamia masuala haya kuelewa na kwenda kusimamia utekelezaji wake," alieleza Kihwele.

Kwa upande wake Mtafiti Mwandamizi kutoka TFNC, Luitfrid Peter, alibainisha kuwa wanawake milioni 3.3 kuanzia umri wa miaka 15 hadi 49 wanakabiliwa na uzio uliokithiri na upungufu wa damu ukitajwa kuwa changamoto kubwa.

"Kwenye nchi za Afrika Mashariki kiwango cha udumavu ni asilimia 31, wakati Shirika la Afya Duniani linapendekeza kiwango cha udumavu kiwe angalau chini ya asilimia 20 kwa hiyo bado tuna kazi kubwa ya kuvuta hiyo namba iwe chini ya asilimia hizo na kulifikia hili ni lazima tushirikiane pamoja na wananchi ambao ndiyo walengwa kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na afya bora," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Sera na Mipango kutoka TFNC, Geoffrey Chiduo, alisema kuwa mikoa 15 inaongoza kwa udumavu yenye zaidi ya asilimia 30 na mikoa 7 ambayo ina asilimia 40 ya watoto ambapo kati ya 10 watoto wanne wana udumavu wakati huo ikitajwa kiwango kikubwa cha uzalishaji wa chakula na uchumi mzuri.

"Tatizo linaweza kuwa siyo uzalishaji wa chakula ila ni kuhusiana uelewa wa masuala ya lishe bora na zipo sababu nyingi ikiwamo aina ya chakula wanacholishwa hao watoto hakina mchanganyiko unaotakiwa," alisema.



# TASAF yashauriwa mkakati ukomo wa wanufaika

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF), umetakiwa kuandaa mkakati wa kuweka ukomo na kuwaondoa wanufaika wa mpango wa taifa wa kunusuru kaya maskini ambao wamefanikiwa kujikwamua kiuchumi ili kutoa fursa ya kuingiza kaya nyingine zenye uhitaji.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, wakati akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwenye kikao cha kamati ya uongozi wa TASAF Taifa, ambayo imetembelea wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini wilayani Rungwe.

Dk. Chuachua alisema TASAF haiwezi kuyafikia maeneo yote kwa wakati mmoja hivyo lazima mkakati uwekwe wa kuwaondoa wanufaika wa mpango huo ambao tayari wamenufaika hapo awali.

Alisema TASAF kwa sasa inatakiwa kuzifikia kaya ambazo bado hazijanufaika kwa kuhakikisha wanapewa fedha za kujikwamua na umaskini ikiwamo kuanzisha miradi ya maeneo kama vile shughuli za ujasiriamali.

"Watu hawa ambao tunasema ni kaya maskini sawa, lakini lazima tuwatoe hapo walipo maana tayari wamenufaika, tuanze kuzifikia kaya nyingine ambazo hazikufikiwa na mpango huo," alisema Dk. Chuachua.

Akizungumzia wito huo, Mkurugenzi wa TASAF, Ladslaus Mwamanga, alisema mpango huo hauwezi kuendelea kuwanufaisha ambao tayari wameingizwa kwenye mpango huo pekee bali wameandaa utaratibu kuendelea kuwatambua wengine kwa kukusanya na kuthibitisha uhakiki wa taarifa zao.

Alisema sambamba na kuandaa utaratibu wa namna ya kuzitambua kaya maskini kwa kuzingatia kanzidata, vilevile, wameendelea kuwahamasisha matumizi sahihi ya fedha zao ikiwamo kuanzisha shughuli za uzalishaji mali kwa kuanzisha vikundi. "Katika mpango wa miaka mitatu hadi mitano, TASAF tunaendelea kuwahamasisha wale wote walioingia kwenye mpango huo sasa kuendelea kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ili fedha hizo ziendelee kuzalisha badala ya kuzitumia kwa matumizi mengine ambayo hayana tija katika kujikwamua na umaskini," alisema Mwamanga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi wa TASAF, Dk. Naftal Ngondi, alisema taarifa ya utekelezaji ya mpango huo katika Mkoa wa Mbeya inakwenda vizuri na kuwapongeza waratibu huku ikiwasisitiza kuwa fedha zinazotolewa ziendelee kuwakwamua wananchi dhidi ya umaskini.

Kwa upande wake, Mratibu wa TASAF Mkoa wa Mbeya, Aika Temu, alisema mpango huo unazinufaisha halmashauri zote saba za mkoa huo na hadi 2022 jumla ya wananchi 5,767 wamepata ruzuku kutoka vijiji 783.

Miongoni mwa wanufaika wa mfuko huo, Sauda Mwamboneke kutoka wilayani Rungwe, alisema amefanikiwa kuanzisha biashara, kusomesha na kujenga nyumba nzuri kupitia fedha hizo.

Aliishukuru TASAF kwa kuwawezesha kujikwamua na umaskini na kuwaahidi kutumia fedha hizo kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo.



Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Mfuko wa Taifa wa Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) wakimpatia zawadi ya fedha mnufaika wa mpango huo, Atupele Kasapa (katikati), mkazi wa Kata ya Ibigi wilayani Rungwe kutokana na matumizi mazuri ya fedha alizokuwa amepatiwa kwa kujenga nyumba na kuanzisha mradi wa kufuga nguruwe mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wafurahia kufikishiwa umeme kijijini

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Mbonile, Kata ya Ulenje wilayani Mbeya, ambao tangu nchi ipate uhuru wamekuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilometa 10 kwenda kusaga nafaka katika vijiji vya jirani, sasa wameondokana na kero hiyo baada ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini (REA), kuwafikishia umeme na kuvutia wawekezaji kupeleka mashine za kusaga nafaka.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni wakazi wa kijiji hicho walisema kwa sasa wanafurahia umeme kijijini hapo kwa kusaga nafaka na kupata huduma nyingine muhimu.

Zainabu Richard, alisema awali walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata nishati ya umeme maeneo ya mbali kusaga nafaka, lakini sasa wanapata huduma zote kwenye eneo lao.

"Tulikuwa tunatembea umbali mrefu kutoka hapa kijijini kwetu kwenda vijiji vingine ikiwamo Maadilisho au Irambo kusaga nafaka zetu tena kinamama tulitembea kwa miguu na watoto mgongoni, tunamshukuru Mungu TANESCO wametuletea umeme sasa tunasaga mahindi hapa," alisema Richard. Gervas Kembo, alisema kwa sasa wananchi wamehamasika kuingiza umeme kwenye makazi yao baada ya Shirika hilo kusogeza huduma hiyo, hata hivyo aliiomba serikali kuendelea kuboresha miundombinu ikiwamo vituo vya afya na zahanati ili huduma za matibabu zipatikane karibu na makazi yao.

Diwani wa Ulenje, Mhandisi Boniface Njombe, aliishukuru serikali kwa kuwasogezea umeme karibu na makazi yao na kwamba uwapo wa huduma hiyo umerahisisha shughuli za ujasiriamali.

Alisema kwa sasa kinamama wako bize kuanzisha shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato na kusaidia kumudu mahitaji ya familia zao ikilinganishwa na ilivyokuwa awali na kushindwa kuongeza thamani ya mazao yao kama vile viazi mviringo. Meneja TANESCO, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Mathia Solongo, alisema miongoni mwa mikakati ya shirika hilo ni kusambaza umeme kwa wananchi.

Alisema kupitia mradi wa REA, Shirika hilo linaendelea kusambaza umeme maeneo yote ya vijijini ambayo hayakufikiwa na huduma hiyo kwa bei elekezi ya Sh. 27,000.

"Lengo letu sisi TANESCO ni kuhakikisha kila siku tunawaunganishia wateja 200 umeme mkoani Mbeya na kwamba tunajipanga kuongeza magenge ya kuongeza nguvu kazi ya kusambaza umeme kwa wakati alisema," Mhandisi Solongo.

## Zaidi ya watoto 200,000 wapatiwa chanjo ya polio

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WATOTO 262,039 wa Mkoa wa Songwe, wamepatiwa chanjo ya kujikinga na polio iliyofanyika kwa siku nne mfululizo kuanzia Machi 24 hadi 27, mwaka huu.

Awali, lengo la utoaji chanjo hiyo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano lilikuwa ni kuwafikia watoto 224,455, lakini kutokana na hamasa waliopata wazazi pamoja na walezi kuhusu umuhimu wa kuwachanja watoto walivuka lengo.

Kwa mujibu wa Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Songwe, Dk. Hamad Nyembea, idadi hiyo ya watoto kuchanjwa imeufanya mkoa kufika lengo la asilimia 117.

"Tunawashukuru sana wazazi pamoja na walezi kwa kuhamasika kuwapatia watoto chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa polio ambao tayari nchi jirani ya Malawi wanapambana nao kuutomeza tumejitahidi kuvuka lengo hii inaonyesha tuko kwenye mapambano kweli kweli," alisema Dk. Nyembea.

Aliongeza kuwa katika zoezi hilo Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, ilichanja watoto 52,259 na kuvuka lengo la 33, 589 sawa na asilimia 156, Mji wa Tunduma ilichanja watoto 40,201 wakati lengo lilikuwa 29,606 sawa na asilimia 136 huku Wilaya ya Ileje iliwafikia watoto 20,008 lengo likiwa ni 23,107 na kufikia asilimia 87.

Alisema Mkoa wa Songwe ulijipanga vyema kwa kutoa elimu kwa wananchi pamoja na watoa huduma 1,874 ambao walijengewa uwezo namna bora ya kuendesha zoezi hilo ambalo lilifanyika nyumba kwa nyumba, vituo vya kutolea huduma, shuleni, misikitini na kwenye makanisa.

Wakati wa zoezi hilo, Mratibu wa chanjo Mkoa wa Songwe, Mosses Lyimo, alisema waliandaa vifaa vya kutosha, wataalamu na timu ya watu watatu katika kila wilaya kusimamia na kuratibu zoezi hilo ambao waligawana majukumu ya kutoa chanjo, kuchanja na kuchukua rekodi za idadi ya watoto watakaochanjwa.

Aidha, alisema baada ya utoaji chanjo kwa siku nne kukamilika imeandaliwa timu ya watu ambao watatembelea makazi ya wananchi kuhakiki na kujiridhisha watoto waliopata.

Hata hivyo, Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Songwe, Dk. Hamad Nyembea, alisema utoaji chanjo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano unaendelea na ambao hawakupata chanjo hiyo wafike kwenye vituo vya kutolea huduma.



# Ataka somo la Historia kurudishwa shuleni

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Maendeleo ya Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pemba Juma, amesema wakati umefika wa kurudisha somo la Historia shuleni ili kuepuka upotoshaji unaofanywa kwa viongozi waasisi wa nchi pamoja na mchango wao wa ujenzi wa taifa katika harakati za Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964.

Waziri Pembe, alisema hayo Chake Chake, Pemba wakati akifungua kongamano la kitaifa la kumuenzi na kutambua mchango wa Rais wa kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume, aliyefariki dunia Aprili 7 mwaka 1972 kwa kuuawa kikatili.

Alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sasa ipo katika mapitio ya mitaala ya elimu na suala la somo la historia linahitaji kuzingatiwa ili kusomeshwa katika shule za msingi na sekondari.

Alifafanua kuwa kitendo cha kutosomesha somo la Historia matokeo yake ni kujitokeza kwa matukio ya upotoshaji wa historia hiyo kwa watu ambao hawaitakii mema Zanzibar.

“Tumezungumza muda mrefu kuhusu umuhimu wa kuanzishwa somo la historia katika mitaala ya elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari...tunafanya mapitio ya mitaala ya elimu ambapo huu ni wakati wake muafaka wa kufanya kazi hiyo,” alisema.

Pembe alisema kifo cha Rais Karume kinawakumbusha wananchi na viongozi uadilifu, uzalendo wa kufanya kazi na kuleta maendeleo.

Alisema katika kipindi kifupi cha uongozi wake wa miaka tisa alifanya mambo makubwa ikiwamo kuondoa ubaguzi wa misingi ya ukabila na kujenga taifa lenye usawa.

Alisema katika kipindi ambacho alikuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ameshuhudia kazi kubwa iliyofanywa na kiongozi huyo jasiri katika kuimarisha elimu kwa mustakabali wa maisha ya vizazi vijavyo.

Alisema katika kuona elimu inamilikiwa na serikali, Rais Karume alitangaza mapema elimu bure, Septemba mwaka 1964 ambayo imetoa fursa kubwa kwa watoto wa wakulima na wakwezi kupata elimu bila ya vikwazo.

Akitoa mada kuhusu mchango wa Karume katika maendeleo, Mwalimu Mkuu mstaafu wa Shule ya Utaani Pemba, Bakari Ali, alisema Hayati Karume ni kiongozi wa kupigiwa mfano ambaye alifikisha maendeleo bila ya ubaguzi kati ya Unguja na Pemba kwa ujenzi wa nyumba za maendeleo hadi vijijini.

“Ni miaka 50 tangu kifo cha Karume ambapo matunda yake tunafaidi wananchi wengi ikiwamo kuishi katika nyumba za ghorofa za maendeleo zilizojengwa Pemba yote na Unguja,” alisema.

# Kilimo viungo, mboga, matunda chawakomboa wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MRADI wa kilimo cha viungo, mboga na matunda ikiwamo bustani za nyumbani unatajwa kuwa mkombozi kwa wanawake.

Mradi huo unaotekelezwa na Shirika la People Development (PDF), Taasisi ya Uhifadhi wa Misitu Pemba na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) upande wa Zanzibar, chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU), ukiwa na lengo la kuwainua wanawake kujiwekeza katika shughuli za kilimo cha viungo, mboga na matunda.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti wakati wa ziara ya kuangalia kilimo cha bustani za majumbani, wanufaika wa mradi huo walisema kuwa kilimo hicho ambacho kimejikita katika mboga na matunda kimekuwa ni mkombozi kwao.

Mariam Juma mkazi wa Kijichi Unguja, alisema kuwa baada ya kujikita katika kilimo hicho familia yake inakula chakula bora ambacho huwa na mboga.

“Hivi sasa hatuli chakula kikavu, nimependa mboga za aina mbalimbali ikiwamo tembele, mchicha, spinach, kisamvu ambapo huuza na pia hutumia kwa ajili ya kuipikia familia yangu,” alisema.

Alisema kuwa kutokana na eneo dogo la ardhi alilonalo nyumbani kwake, ametafuta njia mbadala ya kutumia viroba kwa ajili ya kupanda mboga.

Alisema elimu hiyo ya upandaji wa mboga wamepatiwa kupitia mradi wa viungo na kwa sasa umepunguza gharama ya ununuzi wa mboga.

“Kabla ya kupatiwa elimu ya ukulima wa mboga na matunda kwa kutumia njia mbadala nilikuwa kama sina pesa siwezi kula mboga, lakini kwa sasa nimezungukwa na mboga ya kila aina,” alisema.

Naye Nasra Majid, mkazi wa Kijichi Wilaya ya Magharibi A Unguja, alisema kuwa kilimo hicho hakihitaji maji mengi licha ya kukabiliwa na changamoto ya uhaba wa maji.

Alisema kilimo hicho hawatumii mbolea za kemikali bali za asili pamoja na dawa za asili za kuulia wadudu.

“Mbolea za asili tunazotumia mfano ni kinyesi cha wadudu ikiwamo kuku au ng’ombe na dawa za asili tunazotumia kwa ajili ya kuulia wadudu ni pilipili,” alisema.

Kwa upande wake, Ali Said Juma, Ofisa Kilimo wa mradi wa viungo alisema mradi huo umekuja kuwakomboa wanawake na kuingia katika kilimo cha biashara chenye tija.

Said alisema mradi huo umewasaidia wakulima kuwapatia mbegu za kilimo pamoja na kusogeza huduma za usambazaji wa miundombinu ikiwamo maji.

“Kwa mfano mradi huu umewawezesha wakulima kuwapatia elimu ikiwamo kutengeneza na kuzalisha mbolea asilia isiyokuwa na kemikali,” alisema.



Mariam Juma ni mkulima wa mboga akiwa nyumbani kwake Kijichi. Anajishughulisha na kilimo cha bustani ya nyumbani chini ya mradi wa viungo, mboga na matunda unaotekelezwa na Shirika la People Development (PDF), Taasisi ya Uhifadhi wa Misitu Pemba na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Madereva watakiwa kupakia abiria katika vituo vilivyowekwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Massoud Makame, amewataka madereva wa magari ya abiria na waendesha bodaboda kupakia abiria katika vituo vilivyowekwa kisheria na kujiepusha na tabia ya kupakia abiria katika maeneo yasiyokuwa rasmi.

Akizungumza hivi karibuni katika uzinduzi wa kampeni ya lami salama katika uwanja wa misuka Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema kitendo cha madereva kupakia abiria katika vituo visivyo rasmi ni miongoni mwa sababu zinazosababisha ajali, vifo pamoja na ulemavu.

Aliiomba Wizara ya Mawasiliano kuanzisha vituo vya daladala pamoja na kuweka alama za barabarani ili kupunguza idadi ya ajali katika mkoa huo pamoja na kuwasisitiza wananchi kutumia vituo vilivyoko ili kuondoa msongamano wa magari na kusababisha ajali.

Alisema barabara ni kiunganishi kikubwa cha shughuli mbalimbali za kijamii ambazo kichocheo kizuri cha kuleta maendeleo na kwamba ipo haja kwa kila mtumiaji kuzingatia matumizi sahihi ya barabara ili kila mmoja kutimiza malengo yake.

Pia aliwataka madereva kuacha tabia ya kumwaga mafuta machafu katika barabara na kufanya hivyo kunasababisha kuharibika kwa miundombinu hiyo ambayo serikali imetumia gharama kubwa kuzitengeneza.

Naye Naibu wa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Juma Makungu Juma, alisema wizara yake imejipanga kuhakikisha inaweka alama za barabarani ili kupunguza ajali zinazoepukika.

Alisema ajali nyingi hutokea kutokana na baadhi ya madereva kuendesha vyombo vya moto kutokufuata sheria za usalama barabarani.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema uongozi wa mkoa huo utahakikisha unasimamia kwa kuwachukulia hatua za kisheria madereva watakaobainika kupakia abiria kinyume na matumizi ya leseni zao.

Aliwataka madereva wa bodaboda pamoja na magari ya abiria kukata bima za vyombo vyao ili kuendesha shughuli zao bila ya usumbufu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



SIKUJUA SALAZIERY SALMON anatangaza kupotea cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3680/0092** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari **CHABALISA** mwaka **2010.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: KAG/KAY/RB/124961/2022**

## GARI ZINAUZWA

MAZDA CX7 SPECIAL EDITION (NYEUSI)4WD 2,300 c.c PETROLI IPO KATIKA HALI NZURI.IMETEMBEA 65,000km,TOYOTA CAMI (NYEUSI) 4WD 1,300 c.c PETROLI IPO KATIKA HALI NZURI IMETEMBEA 115,000km

**KWA MAWASILIANO NAMBARI:0737 708 890/0755 378 346**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe
Kituo cha Njombe Mjini
Mkoa Njombe

Usimamizi wa Mirathi Na. 26/2022
Katika Shauri la Mirathi ya
AUGUSTINO SALIMU HONGOLE...............Marehemu
Wa Njombe

Katika Shauri la maombi ya kumteua Msimamizi yaliyoletwa na
HANS AUGUSTINO HONGOLI..................Mwombaji

**TANGAZO KWA UMMA**
(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 30 Mwezi 04 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 30 Mwezi 3 Mwaka 2022.**

HAKIMU MKAZI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

PEST GUARD LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye namba za USAJILI NAMBA T101 APB, CHASSIS NAMBA JTEHC006J104011915, ENGINE NAMBA 1HD0238072. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
TAARIFA POLISI: DAR/CEN/RB/133981/2022

## MAJEMBE AUCTION MART (S.L.P 196 IRINGA)

Tunaomba kuutangazia umma juu yam nada wa hadhara wa mali za wadai wa Shirika la Nyumba la Nyumba la Taifa Mkoa wa Iringa. Mnada utafanyika tarehe 16/04/2022 majira ya saa tano asubuh maeneo ya Kihesa Majembe(Iringa).

**Mali zitakazouzwa ni za wadaiwa wafuatao:**

| S/N | JINA LA MDAIWA | NYUMBA ALIYOKUWA AMEPANGA | MALI ZINAZOUZWA |
|---|---|---|---|
| 1 | DENNIS EMMA BAHATI (BACKYARD LOUGE) | NA. 015(Plot 4B/ II) | MALI MBALIMBALI |
| 2 | REGINA H. KESSY | NA. 013(PLOT 4A/II) | MALI MBALIMBALI |
| 3 | RUKIA MKUMBO | NA. 019(PLOT 8/II) | MALI MBALIMBALI |
| 4 | IBRAHIM H. NGENG'NA | NA.063(PLOT4.090/HKT) | MALI MBALIMBALI |
| 5 | TADEO A. MWAMPOKA | NA.066(PLOT 4.090/HKT) | MALI MBALIMBALI |

MASHARTI YA MUDA
- UKAGUZI UNARUHUSIWA SIKU MBILI KABLA YA SIKU YA MNADA.
- MNUNUZI ATALIPA FEDHA TASLIMU(CASH)

**MAWASILIANO**
- OBADIA MOTTO...............................0755 976 676
- KIMBAMA TWAHA............................0627 233 080
- ALPHONCE PANGISA.........................0655 136 010
- SETH MOTTTO..................................0764 464 746

IN THE RESIDENT COURT
OF GEITA AT GEITA
MISC/EXCUTION/CIVIL/ APPLICATION /PROBATE CAUSE CASE NO 3 OF 2022
THE BOARD OF TRUSTEE PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND...DECREE HOLDER
VERSUS
1. NYARUGUSU MINE CO.LTD....JUDGEMENT DEBTOR
2. MANAGING DIRECTOR NYARUGUSU MINE CO. LTD...JUDGEMENT DEBTOR

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT,** the above case has been fixed for hearing/mention on the 13th day of APRIL,2022 at 8:30AM. in the forenoon .
**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
**GIVEN UNDER** under my hand and the **SEAL** of the Court this **23th day of MARCH, 2022.**

PRINCIPAL /SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE
TO BE SERVED UPON.

**1. NYARUGUSU MINE CO.LTD. Signature..........**

**2. MANAGING DIRECTOR NYARUGUSU MINE CO.LTD.......Signature**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE GEITA

IN THE HIGH COURT OF
THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA
LAND CASE APPEAL No. 58/2021

Arising from the District Land and Housing land application 30/2014

BENEDICTO LUKWEMBE .........................APPELLANT
VERSUS
DESDERY NGAIZA .................2ND RESPONDENT
ANETH MSAFIRI ....................3RD RESPONDENT

TO,
ANETH MSAFIRI

**RE NOTICE FOR DATE OF HEARING**

Whereas the above mentioned APPELLANT has lodged a case registered as Misc Land case Appeal no. 58/2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been scheduled for hearing on 27th day of April, 2022 at 08:30 am before Hone Mwipopo J. You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 28th day of March, 2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ZAITUN ADAM SAKURU **ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **GARI (TOYOTA-PASSO)** yenye namba za usajili **T900 DFY** Chassis namba: **QNC100006527** Injini namba : 1241359 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/115930/2022

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 39 OF 2022**

In the Matter of the Estate of the Late LUPONELO FUPI NGULO
By 1. EVA LUTENGAMASO MGENI
2. ..........................................
All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 06 day of 04. 2022
Dated at MOROGORO this 23 day of 03.........2022

**RESIDENT MAGISTRATED**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MARYSIANA ELIAZAR ERNEST anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RAUM yenye NAMBA ZA USAJILI T201 DSH ,CHASSIS NAMBA NCZ20-0043764 POLISI CONTROL NAMBA : 9910832492451

ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI – DODOMA TUTAFANYA MNADA WA HADHARA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 09/04/2022 KUANZIA SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA NYUMBA MOJA PLOT No. 25 BLOCK "B" ILIYOPO KISASA MSANGALALE SQ 700 MALI YA WANANDOA IDD HUSSEIN OYE NA SOPHIA H. ABDULRAHMAN KWA SHAURI LA MADAI YA TALAKA NO.13/2021.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI TUPIGIE. NO. 0713913150.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**KITUO CHA KIHONDA, MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA Na.15...2022**
**JINA LA MDAI: YOUZE N KASHANGA**
**JINA LA MDAIWA: SARAH ISRAEL MKUMBO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: SARAH ISRAEL MKUMBO ALIYEPO KAHAMA MKOA WA SHINYANGA.

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:kuomba ndoa ivunjwe,mgawanyo wa mali na matunzo ya motto.Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 06/04/2022 saa 03:asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO:Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 01/04/2022**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA



Baadhi ya washukiwa 17 wanaodaiwa kuhusika na shambulizi dhidi ya Raila Odinga. Miongoni mwa mashtaka wanayokabiliwa nayo ni pamoja na jaribio la mauaji, uchochezi wa ghasia, uharibifu wa mali na uvunjifu wa amani. **PICHA: NATION MEDIA GROUP**

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

# Waliomshambulia Odinga kwa mawe wakabiliwa mashtaka mauaji

**Nairobi,** KENYA

WASHUKIWA 17 wamefikishwa mahakamani Eldoret wakihusishwa na shambulizi dhidi ya mgombea urais kupitia muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya, Raila Odinga, lililotokea eneo la Kabenes, Kaunti ya Uasin Gishu, mwishoni mwa wiki.

Washukiwa hao wanadaiwa kuhusika na shambulizi la kupiga mawe helikopta iliyokuwa imembeba Raila, kiongozi wa ODM, ambaye ni kiongozi wa Chama cha ODM, eneo la shamba la marehemu Mzee Jackson Kibor la Samitui, muda mfupi baada ya mazishi.

Miongoni mwa mashtaka dhidi yao ni pamoja na jaribio la mauaji, uchochezi wa ghasia, uharibifu wa mali na uvunjifu wa amani.

Washukiwa hao watashikiliwa kwa siku 14, mahabusu ili kuruhusu uchunguzi kukamilika.

Odinga alitembelea shughuli za mazishi na kukumbwa na tukio hilo.

Mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Mashtaka (DCI) alisema uchunguzi wa awali umeanza na kwamba wabunge wawili akiwamo wa Soi, Caleb Kositany na mwenzake wa kaunti ya Uasin Gishu, David Kiplagat, walihojiwa eneo la makao makuu ofisi ya DCI Nakuru.

Rais Uhuru Kenyatta alilaani tukio hilo akisema linahatarisha amani na usalama wa nchi na linaweza kuchochea uvunjifu wa amani.

Raila Odinga anayewania urais kupitia Azimio la Umoja One Kenya amelaumu shambulio dhidi yake akiwa katika helikopta eneo la Kabenes, Kaunti ya Uasin Gishu.

Raila ameendelea na kampeni kuelekea uchaguzi mkuu Agosti mwaka huu.

Amesema kundi la vijana lilimvamia wakati akiondoka eneo hilo kuelekea Ortum, Alale na Lomut, kuendelea na kampeni.

Amedai kwamba mawe yalirushwa akiwa pamoja na ujumbe wake.

Amesema hata wakati akielekea kupanda helikopta mawe yaliendelea kurushwa.

"Sisi hatujapiga mtu yeyote. Wala hatujafanya fujo pahali popote, tunalaani. Jana mimi nimeona vioja. Vijana wanakuja sisi tulitoka kutoa pole kwa familia halafu wakaanza kupiga magari yetu mawe.

"Mawe yalinyesha kama mvua kwenye gari langu. Wakipiga, nikauliza ni nini kinafanyika. Vijana wakangoja nikiingia kwenye ndege halafu nikaona mtu anarusha mwamba mkubwa na sikuwa na pahali pa kuenda. Nilishangaa, ni mambo gani haya. Jamaa walitaka kutuua sisi."

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Papa awaenzi waandishi wa habari waliouawa Ukraine

**Kyiv,** UKRAINE

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis (pichani), amewaenzi waandishi wa habari waliouawa katika vita vya Ukraine akisema anatumai Mwenyezi Mungu atawapa malipo kwa kuwatumikia kwa wema watu wote bila kujali ni upande gani wanatokea.

Akizungumza na wanahabari akiwa ndani ya ndege akirejea kutoka Malta, Francis ameeleza kwa mara nyingine kwamba yuko tayari kufanya ziara katika mji mkuu wa Ukraine, Kyiv, lakini akiongeza kuwa hajaamua iwapo hilo litawezekana.

"Nataka kutoa rambirambi kwa wenzenu walioaga dunia, bila kujali upande wanakotokea," amesema.

"Kazi yenu ni kazi kwa manufaa ya watu wote. Walifariki wakiwa wanafanya kazi kwa ajili ya manufaa ya watu wote kupata habari. Tusisahau kwamba walikuwa na ushujaa. Ninawaombea, ninamwomba Mola awalipe kwa kazi yao."

Wanahabari sita waliuawa tangu majeshi ya Russia yalipoivamia Ukraine mwishoni mwa mwezi Februari.

Francis amesema pia kwamba amekuwa akipata habari kuhusu Ukraine kwa mawasiliano ya simu kila baada ya siku chache na mwandishi wa



habari wa Argentina anayeishi Roma Elisabetta Pique, rafiki yake wa karibu ambaye amekuwa akiripoti vita vya Ukraine tangu mwanzo.

Akiwa njiani kuelekea Malta Jumamosi, Francis alisema safari ya kwenda Kyiv ipo kwenye ratiba.

"Niko tayari kufanya lolote linalowezekana. Vatican inafanya kila kitu kwa upande wa kidiplomasia.

"Kwa sababu za busara na usiri, hatuwezi kutangaza kila kitu hadharani," alisema akiwa ndani ya ndege.

Ukraine imeshutumu wanajeshi wa Russia kwa mauaji ya kimakusudi baada ya miili ya watu wasiopungua 20 waliovalia nguo za kiraia kupatikana mitaani katika mji huo.

Mamia ya maiti zinasemekana kupatikana katika miji ya nje ya mji wa Kyiv kufuatia kuondoka kwa wanajeshi wa Urusi katika eneo hilo, kwa mujibu wa maofisa wa Ukraine. Russia inakanusha mauaji yoyote.

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, ametoa wito wa kuwekewa vikwazo zaidi vinavyolenga mauzo ya makaa ya mawe na mafuta ya Russia, akiviambia vyombo vya habari vya Ufaransa kuna ushahidi wa wazi uhalifu wa kivita.

Waziri wa Ulinzi wa Ujerumani, Christine Lambrecht, anasema Umoja wa Ulaya lazima sasa ujadili kupiga marufuku uagizaji wa gesi ya Russia, jambo ambalo viongozi wamesita kufanya hadi sasa licha ya kuhimizwa na Ukraine kwa sababu ya athari ambayo ingekuwa kwa watumiaji wa Ulaya. Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ameeleza picha za maiti kuwa ni pigo tumboni.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, alilaani kile alichokiita mashambulizi ya yenye ukatili. Ripoti zinaonyesha kuwa Uingereza inaweza kutangaza vikwazo vipya wiki hii.

Wakati huo huo, Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, alisema vikwazo na uungwaji mkono zaidi wa Umoja wa Ulaya ziko njiani.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

# NAMUNGO, KAGERA ZALIA NA JUA KALI KUWAATHIRI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Namungo na Kagera Sugar zimedai joto kali lililotokana na jua kwenye mechi zao za Ligi Kuu ni moja ya sababu zilizoathiri matokeo yao juzi.

Namungo ikiwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ilitoka suluhu na wenyeji wao KMC katika mchezo uliopigwa saa kumi jioni, huku Kagera Sugar ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye mechi ya 'dabi' ya Sukari, iliyochezwa saa nane mchana kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Straika wa Namungo FC, David Molinga, alisema mechi ilikuwa nzuri, lakini jua lilikuwa kali sana na kusababisha kapeti la Uwanja wa Uhuru kuwa na joto lililokithiri.

"Tumecheza vizuri, KMC pia ni timu nzuri sana, ila leo jua lilikuwa kali sana, kwa hiyo kulikuwa na joto sana, pia hili kapeti la Uwanja wa Uhuru likashika joto hali iliyosababisha wachezaji wa timu zote tuchoke na tucheze kwenye changamoto kubwa, hivyo kupata pointi moja kila timu, hasa sisi siyo mbaya kwa sababu tuko ugenini," alisema straika huyo wa zamani wa Yanga.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar iliyotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa, Francis Baraza, alisema wachezaji wake walicheza mechi hiyo saa nane mchana, wakipitia kwenye mateso makali kutokana na joto kali lililotokana na jua.

"Haikuwa mechi rahisi, hawa jamaa wako sehemu mbaya wanatafuta kujinasua na walipata nafasi nyingi kipindi cha kwanza, wakashindwa kuzitumia. Pongezi kubwa kwa wachezaji wangu, kwanza wanajua sana kuzicheza hizi mechi za ugenini, na hii kupata pointi moja si mbaya kwa sababu kwanza baadhi walikuwa wamefunga, halafu wamecheza kwenye jua kali, kulikuwa na joto sana kwa sababu mechi imechezwa saa nane, ilikuwa ni kama wanapitia kwenye mateso makali," alisema kocha huyo.

IKO HIVI...




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akimwelekeza jambo mchezaji mwenza wa timu hiyo, Yusuph Athumani katika mazoezi ya timu hiyo kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC, itakayopigwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

# *Nusu Fainali FA Cup Z'bar kupigwa Mei*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup hatua ya nusu fainali imepangwa kuchezwa kuanzia Mei 10 -11, mwaka huu kwa upande wa Kanda ya Unguja.

Nusu fainali ya kwanza itachezwa Mei 10, kwa timu ya New King kuikaribisha Kipanga FC wakati nusu fainali ya pili ikichezwa kesho yake kwa Zimamoto kuvaana na Maafande wa Mafunzo.

Mechi zote zitachezwa majira ya saa kumi alasiri katika Uwanja wa Amaan.

Akizungumza na viongozi wa klabu zilizoingia hatua ya nusu fainali, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano, Ali Bakari 'Cheupe', alisema hatua hiyo itachezwa kabla ya mwendelezo wa Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ambapo zote zimesimama kupisha mwezi wa Ramadhani.

Alisema hatua ya nusu fainali kwa Kanda ya Unguja, itapangwa baada ya kushauriana na Bodi ya Ligi ili kuepusha mwingiliano wa ratiba kwa Ligi Kuu na Kanda.

"Leo tumeziita klabu ambazo zimeingia hatua ya nusu fainali, lengo ni kupanga kwa pamoja juu ya kuchezwa mechi za nusu fainali mbili, awali kulikuwa na mapendekeza kuwa tuendelee na FA katika kumi la mwisho la mfungo wa Ramadhani, lakini klabu zimependekeza bora imalizike Ramadhani na tumeafikiana hivyo," alisema.

Hata hivyo, alizitaka klabu kujiandaa na hatua hiyo ya nusu fainali, na fainali ya kwanza kwa Kanda ya Unguja na ile ya Mwisho ambayo itakutanisha mshindi wa Kanda ya Unguja na Pemba.

# European Gofu Tour sasa hadi mwakani

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

MASHINDANO ya European Tour ya mchezo wa gofu yaliyokuwa yafanyike Aprili 7-10, mwaka huu jijini Arusha yamesogezwa mbele hadi Februari mwakani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Chris Martin, alisema mashindano hayo yamesogezwa mbele kutokana na baadhi ya washiriki kutotimiza taratibu walizokuwa wamejiwekea.

**"Tunasikitika kusogezwa mbele kwa mashindano haya kwa sababu washiriki walikuwa wamejiandaa kwa kipindi kirefu, tunaomba radhi kwa kampuni na taasisi zote zilizokuwa zimetudhamini," alisema Martin.**

Alisema wiki hii wanatarajia kukutana na Wizara ya Michezo, Utamaduni na Sanaa kwa lengo la kupanga mikakati na kwamba baada ya kikao hicho wataiweka bayana ili Watanzania wafahamu kinachoendelea.

Mwenyekiti huyo alisema kwa sababu ya ukubwa wa mashindano hayo, ingekuwa ni mara ya kwanza kufanyika hapa nchini, hivyo imewawia vigumu kutoa taarifa hizo.

# KMC hesabu zote kwa Kagera Sugar

**Na shufaa Lyimo**

BAADA ya kutoridhishwa na matokeo ya sare dhidi ya Namungo FC, sasa maandalizi motomoto kuelekea mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar yameanza rasmi, limeeleza Benchi la Ufundi la KMC.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana baada ya mchezo huo, Kocha Mkuu wa KMC, Thierry Hitimana, alisema mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkali kwa kila timu, lakini wachezaji wake walipata nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia.

"Mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani, lakini hatujakata tamaa tunajipanga kwa ajili ya michezo ijayo," alisema Hitimana.

Hata hivyo, Hitimana ambaye anakabiliwa na kibarua kigumu cha kuiongoza timu yake dhidi ya Kagera Sugar kwenye mchezo ujao hapo Aprili 17, mwaka huu, alikiri kwamba ligi msimu huu imekuwa na ushindani mkubwa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**HAALAND KUAMUA MOJA**
MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, ataamua kufikia mwisho wa Aprili ikiwa atajiunga na Real Madrid, Barcelona au Manchester City msimu huu wa majira ya joto. (***Sport***)

**VILLA KUMNUNUA PHILLIPS**
ASTON Villa itashinikiza kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Leeds United na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26, kwa pauni milioni 60 msimu huu. (***Telegraph***)

**AKANJI AITAMANI EPL**
NYOTA anayelengwa na Manchester United, Manuel Akanji mwenye umri wa miaka 26, anataka kuondoka Borussia Dortmund na beki huyo wa Uswisi anafikiria kuhamia Ligi Kuu England. (***Sport1***)

**RUDIGER, BARCA KUTETA**
BARCELONA hawako tayari kutimiza matakwa ya awali ya kifedha ya Antonio Rudiger, lakini watakuwa na mkutano mwingine na beki huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 29, kuhusu uhamisho wa bure kutoka Chelsea msimu huu wa majira ya joto. (***Sport***)

**MARTINEZ PAUNI MILIONI 80**
ARSENAL na Tottenham wanavutiwa na Lautaro Martinez, lakini Inter Milan itamuuza tu mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 24, ikiwa watapokea ofa ya zaidi ya euro milioni 80. (***Calciomercato***)

**FABIANSKI KUWEKWA SOKONI**
KLABU ya West Ham itamtuza golikipa wa Poland, Lukasz Fabianski mwenye umri wa miaka 36, kwa mkataba mpya msimu ujao. (***Mail***)

**EL GHAZI KUBAKI VILLA**
KLABU ya Aston Villa itajaribu kupata uhamisho wa kudumu kwa Anwar El Ghazi msimu huu wa majira ya joto, lakini Everton hawana mpango wa kumsajili winga huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 26, wakati muda wake wa mkopo na Toffees hao utakapomalizika. (***Football Insider***)

**ARAUJO KUFUNGWA BARCA**
BARCELONA wanataka kuafiki kuongeza mkataba kwa Ronald Araujo, ambaye amepokea ofa kutoka kwa Manchester United, lakini mlinzi huyo wa kati wa Uruguay, mwenye umri wa miaka 23, hajachukulia kwa uzuri Barca kumwania Antonio Rudiger na mlinzi wa Chelsea, Andreas Christensen, 25. (***Sport***)

**THOMPSON ADA KUBWA**
KLABU ya Derby County huenda ikatoza ada kubwa kwa mlinda mlango, Jack Thompson mwenye umri wa miaka 15, huku Manchester City, Tottenham na Chelsea zikiwa na nia ya kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa England. (***Sun***)

**NEWCASTLE YAMTAKA SANCHEZ**
NEWCASTLE wanapanga kutoa ofa ya pauni milioni 20 kwa Brighton kwa mlinda mlango wa Hispania, Robert Sanchez mwenye umri wa miaka 24, msimu wa majira ya joto na pia wanamlenga winga wa Watford raia wa Senegal, Ismaila Sarr, 24. (***Sun***)

**EVERTON KUMRUHUSU ALLAN**
EVERTON itamruhusu Allan aondoke msimu wa majira ya joto, licha ya kiungo huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 31, kubakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake. (***Sun***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI: MBIO ZA UBINGWA LALIGA HAKUNA KUKOMA

**Huu ni wakati mzuri zaidi wa msimu, tutaendelea kulipambania taji hadi...**

**BARCELNA,** HISPANIA

XAVI ameahidi Barcelona "itaendelea kupambana" hadi ionekana kimahesabu kwamba haiwezekani kushinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya Jumapili kujivuta hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Sevilla kwenye Uwanja wa Camp Nou ulikuja kutokana na bao lililofungwa na Pedri, na uliwashuhudia Barca wakiwaruka wapinzani wao Atletico Madrid na kupanda nafasi ya pili.

Wamepitwa pointi 12 na vinara Real Madrid, lakini Barca walimaliza mfululizo wa mechi 15 za Sevilla bila kushindwa kwenye ligi, na sasa hawajashindwa katika mechi 14 za LaLiga.

Akizungumza baada ya ushindi huo, Xavi alikuwa na furaha licha ya pengo kubwa kati ya timu yake na Madrid, ambao Barcelona waliwazaba mabao 4-0 pale Santiago Bernabeu katika mchezo wao wa mwisho ugenini.

> **"Nina maoni mazuri, ninaamini katika kazi, juhudi, kujitolea na kazi ya pamoja," Xavi aliwaambia waandishi wa habari.**

"Sisi ni wazuri sana tunaunga mkono sote tunafanya kazi tunakimbia kwa msingi huu matokeo yaje.

"Huu ni wakati mzuri zaidi wa msimu huu. Tumemtawala mpinzani mkubwa, tukiwa na ulinzi bora katika LaLiga. (Sevilla) ni timu bora, na (Julen) Lopetegui ni kocha mzuri."

Xavi alisema timu yake haikufikiria "kutuma ujumbe", lakini alifurahishwa na juhudi za mashabiki na kusisitiza kuwa wachezaji watajaribu kuifukuza Madrid.

"Hatukutuma ujumbe kwa mtu yeyote," aliongeza. "Tuliutuma kwetu. Tulishinda na kufurahia.

"Hali ilikuwa ya ajabu. Na katika LaLiga, mradi tu namba hazisemi vinginevyo, tutaendelea kupambana."

Pia Xavi alikuwa na maneno ya kumsifu Pedri kwamba "hana wa kulinganishwa".

"Yeye ni mchezaji bora," alisema Xavi kwa shauku. "Amefunga bao lisilo la kawaida. Analeta mabadiliko. Ni furaha kumwangalia akicheza, na ana umri wa miaka 19 pekee.

"Haishangazi. Hana wakulinganishwa. Ninamhimiza kucheza."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,119

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
ATLETICO MADRID
1 | 1.40
X | 4.47
2 | 7.45

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# VAN GAAL ASUMBULIWA TEZI DUME

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal amesema kwamba, anapokea matibabu ya saratani ya tezi dume.

Mholanzi huyo ambaye kwa sasa anaiongoza Timu ya Taifa ya Uholanzi, alitoa tangazo hilo kwenye Kipindi cha Televisheni cha Humberto, Jumapili.

Van Gaal mwenye umri wa miaka 70, alisemaameficha habari hizo kutoka kwa wachezaji wake wakati wa mapumziko ya hivi majuzi ya kimataifa.

"Sikutaka kuwaambia wachezaji wangu kwa sababu ingeweza kuathiri uchezaji wao," alisema.

Van Gaal yuko katika kipindi chake cha tatu kama kocha mkuu wa Uholanzi, akiwa ameiongoza hadi nafasi ya tatu kwenye Kombe la Dunia la mwaka 2014 na sasa kwenye fainali za 2022 huko Qatar.

Aliongeza: "Katika kila kipindi nikiwa kocha wa timu ya taifa nililazimika kuondoka usiku kwenda hospitali bila wachezaji kujua hadi sasa, huku wakidhani ni mzima wa afya, lakini...sipo. "

Katika kipindi cha miaka miwili akiwa Man United, Van Gaal aliiongoza kufanikiwa kubeba Kombe la FA mwaka 2016 kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Jose Mourinho.

Pia, ameshinda mataji ya ligi akiwa na Barcelona, Bayern Munich, AZ Alkmaar na Ajax, ambapo aliiongoza timu hiyo ya Uholanzi kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 1995.

## *Allegri aitoa Juve mbizo ubingwa*

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri amekubali nafasi ya timu yake ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, imetoweka baada ya kupoteza kwa bao 1-0 wakiwa nyumbani dhidi ya Inter Milan.

Wenyeji walidhibiti sehemu kubwa ya pambano hilo, wakimaliza kwa mikwaju 23 ikilinganishwa na mitano tu kutoka kwa Inter, lakini hawakuweza kupata bao.

Bao hilo lilizaa utata huku mkwaju wa penalti wa Hakan Calhanoglu ukiokolewa katika muda wa dakika za lala salama, kabla ya VAR na mwamuzi kuamua irudiwe baada ya wachezaji wengine kuingia kwenye eneo la hatari mapema mno, na kusababisha penalti hiyo kupigwa tena.

Calhanoglu hakufanya makosa mara ya pili, akapiga shuti lake kwenye kona ya chini kushoto na kujaa wavuni.

Akizungumza na DAZN baada ya kupoteza mchezo huo, Allegri alisema matokeo hayo yanaashiria mwisho wa matumaini ya Juventus kuwania taji la Ligi Kuu ya Italia, Scudetto, mwaka huu.

"Kuanzia sasa tunaweza kusema kwamba Juventus wametolewa kabisa kwenye mbio za Scudetto," alisema.



,012,860

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/04/22 | 17:00 | Watford vs Leeds | 2.75 | 3.29 | 2.49 |
| 02. 09/04/22 | 17:00 | Preston vs QPR | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 09/04/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.63 | 3.13 | 2.63 |
| 04. 09/04/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Union Berlin | 2.69 | 3.19 | 2.59 |
| 05. 09/04/22 | 20:00 | Amiens vs Bastia | 2.63 | 2.93 | 2.78 |
| 06. 10/04/22 | 15:15 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.37 | 3.48 | 2.73 |
| 07. 10/04/22 | 16:00 | Sivasspor vs Basaksehir | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 10/04/22 | 16:00 | Brentford vs West Ham | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 10/04/22 | 16:00 | Norwich City vs Burnley | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 10. 10/04/22 | 16:00 | Brest vs Nantes | 2.43 | 3.22 | 2.92 |
| 11. 10/04/22 | 17:15 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.78 | 3.13 | 2.63 |
| 12. 10/04/22 | 17:30 | St. Gallen vs FC Basel | 2.39 | 3.53 | 2.68 |
| 13. 10/04/22 | 20:00 | Strasbourg vs Lyon | 2.60 | 3.30 | 2.65 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 05/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5271 | Jeju Utd vs Ulsan Hyundai | 2.88 | 3.12 | 2.31 |
| 14:35 | 5697 | Sreenidi Deccan FC vs Gokulam Kerala FC | 2.73 | 3.26 | 2.35 |
| 15:00 | 2957 | Ipswich U23 vs Hull City U23 | 1.65 | 4.00 | 4.10 |
| 15:00 | 3007 | Bristol City U23 vs Watford U23 | 1.36 | 5.05 | 6.02 |
| 15:00 | 4337 | QPR U23 vs Sheffield United U23 | 3.50 | 3.79 | 1.82 |
| 15:00 | 5415 | Cardiff City U23 vs Barnsley U23 | 1.60 | 4.09 | 4.38 |
| 17:00 | 5693 | Pogon Grodzisk Mazowiecki vs Pogon Siedlce | 2.26 | 3.25 | 2.86 |
| 17:30 | 1229 | Taborsko vs Sparta Prague B | 2.68 | 3.17 | 2.43 |
| 17:30 | 3014 | SK Prostejov vs Vyskov | 1.95 | 3.27 | 3.56 |
| 17:35 | 4087 | Aizawl FC vs Tiddim Road Athlectic Club | 2.25 | 3.21 | 2.92 |
| 18:00 | 5530 | Juventus Youth vs Hellas Verona Youth | 1.52 | 4.40 | 5.40 |
| 18:30 | 3710 | SuperSport Utd vs Chippa Utd | 2.07 | 2.98 | 3.82 |
| 18:45 | 2338 | Shahrdari Astara vs Esteghlal Mollasani | 2.17 | 2.77 | 3.60 |
| 19:00 | 3008 | Resovia Rzeszow vs Stomil Olsztyn | 1.98 | 3.16 | 3.59 |
| 19:00 | 3276 | Olimpia Grudziadz vs Lech Poznan | 22.32 | 6.60 | 1.11 |
| 19:00 | 3435 | Sandecja vs GKS Jastrzebie Zdroj | 1.37 | 4.29 | 7.21 |
| 19:30 | 4023 | Hamburger SV vs Erzgebirge Aue | 1.39 | 4.85 | 6.54 |
| 20:00 | 2123 | Orgryte IS vs Halmstads BK | 2.84 | 3.19 | 2.53 |
| 20:00 | 2790 | Pordenone vs Frosinone | 3.82 | 3.23 | 1.97 |
| 20:00 | 2867 | Reggina vs Benevento | 2.88 | 3.13 | 2.42 |
| 20:00 | 3115 | Spal vs Cosenza | 1.88 | 3.32 | 4.07 |
| 20:00 | 3701 | Cremonese vs Alessandria | 1.63 | 3.66 | 5.15 |
| 20:00 | 4688 | Ternana vs Lecce | 2.19 | 3.16 | 3.26 |
| 21:00 | 1869 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Baniyas | 2.49 | 3.37 | 2.49 |
| 21:00 | 3168 | Al Ain vs Al Wasl Dubai | 1.32 | 5.07 | 7.02 |
| 21:00 | 5558 | Boulogne vs Bastia Borgo | 2.36 | 3.05 | 3.00 |
| 21:30 | 1475 | Korona Kielce vs Podbeskidzie Bie | 2.58 | 3.02 | 2.63 |
| 21:45 | 1153 | Dagenham and Redbridge vs Boreham Wood | 2.15 | 3.25 | 3.20 |
| 21:45 | 1224 | Wealdstone vs Maidenhead U | 2.30 | 3.26 | 2.91 |
| 21:45 | 1339 | MK Dons vs Crewe | 1.32 | 4.95 | 8.51 |
| 21:45 | 1552 | Sligo Rovers vs Bohemians FC | 2.42 | 3.01 | 2.82 |
| 21:45 | 2542 | Cambridge Utd vs Wycombe | 3.53 | 3.28 | 2.04 |
| 21:45 | 2724 | Morecambe vs Oxford Utd | 3.86 | 3.52 | 1.86 |
| 21:45 | 2729 | Fleetwood Town vs Lincoln | 2.57 | 3.11 | 2.71 |
| 21:45 | 2740 | Forest Green vs Mansfield | 1.97 | 3.36 | 3.66 |
| 21:45 | 2971 | Portadown FC vs Cliftonville Belfast | 6.81 | 4.57 | 1.36 |
| 21:45 | 3425 | Peterborough vs Luton Town | 3.86 | 3.31 | 1.93 |
| 21:45 | 4104 | Wrexham vs Barnet | 1.29 | 5.14 | 8.50 |
| 21:45 | 5100 | Kings Lynn vs Bromley | 3.89 | 3.59 | 1.82 |
| 21:45 | 5117 | Preston vs Blackpool | 2.02 | 3.26 | 3.61 |
| 21:45 | 5171 | Wigan vs Accrington | 1.55 | 3.91 | 5.54 |
| 21:45 | 5227 | Halifax vs Solihull Moors | 2.19 | 3.40 | 3.00 |
| 21:45 | 5234 | Salford City vs Port Vale | 2.52 | 3.06 | 2.81 |
| 21:45 | 5517 | Millwall vs Swansea | 2.21 | 3.12 | 3.27 |
| 21:45 | 5677 | Sheffield Utd vs QPR | 1.70 | 3.62 | 4.66 |
| 21:45 | 5806 | AFC Wimbledon vs Charlton | 2.77 | 3.11 | 2.52 |
| 22:00 | 4220 | Bolton vs Portsmouth | 2.14 | 3.27 | 3.27 |
| 22:00 | 4734 | Manchester City vs Atletico Madrid | 1.40 | 4.47 | 7.45 |
| 22:00 | 5148 | Reading vs Stoke City | 2.66 | 3.11 | 2.61 |
| 22:00 | 5775 | Benfica vs Liverpool | 8.27 | 4.64 | 1.38 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# PABLO ASIFU MASHABIKI KUWAPELEKA ROBO FAINALI



**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amewavulia kofia mashabiki wa Simba waliojazana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi kuwapa hamasa wachezaji, akidai kuwa wamechangia kwa kiasi kikubwa timu kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika juzi usiku, akisema ushindi huo anaupeleka ramsi kwao.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, Simba ikipata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya US Berkane ya Niger, Pablo raia ya Hispania alisema mashabiki wa timu hiyo, pamoja na changamoto ya usafiri mgumu na muda wa mchezo kuanza na kumalizika usiku mkubwa, lakini walijazana uwanjani bila kujali chochote na kuwa bega kwa bega na timu yao kuhamasisha kwa ngoma na kushangilia.

"Hongera kwa wachezaji, klabu na watu waliojitokeza leo, kuna wakati ilikuwa ngumu hata kusikilizana wenyewe kwa wenyewe kwa kelele nyingi walizopiga, lakini kwangu mimi ni vizuri kuungwa mkono kiasi hiki.

"Mashabiki walikuwa wengi sana kwa muda huu wa usiku sana wamekutana na changamoto nyingi wakati wa kuja uwanjani, nafikiri hata wakati wa kurudi, hata asubuhi kwenda kazini, nafikiri huu ushindi ni kwa ajili yao, nashukuru kwa kile tulichokikamilisha.

"Mnaweza kuwa hamjui mambo mengi, lakini miezi ya karibuni imekuwa migumu kwetu tulikutana na magumu mengi, lakini ushindi umetufariji," alisema kocha huyo.

Pablo alisema kwenye Kundi lao la D, bila kupepesa macho, RS Berkane na Asec Mimosas ndizo zilikuwa timu bora zaidi yao, hivyo Simba kwenda robo fainali ni jambo la faraja kwa sababu walikuwa kwenye kundi la timu ambazo zina bajeti kubwa, uwezo wa kifedha, pamoja na viwango vikubwa vya wachezaji wao ambavyo vinawawezesha kucheza hata Ulaya.

"Kwa sasa tunakwenda kucheza na moja ya timu zilizoongoza kwenye makundi kwa kumaliza wa kwanza, lakini sisi tunataka kwenda mbele tuone itakuwaje," alisema Pablo.

Akiizungumzia mechi hiyo, alisema walicheza vema vipindi vyote, lakini hawakuwa makini kipindi cha kwanza.

"Kipindi cha kwanza tulicheza vema, lakini tulikutana na tatizo lile lile linalotusumbua ziku zote kwenye michuano hii, nayo ni kushindwa kuzitumia nafasi. Kipindi cha pili tulicheza vile vile kama cha kwanza, lakini tukawa makini zaidi," alisema.

# Adebayor apewa heshima Simba

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa Simba wamempa heshima kubwa winga mshambuliaji hatari wa US Gendarmerie ya Niger, Victorien Adebayor baada ya juzi kuanza kumuimba na kumkaribisha kwa mara nyingine kuja kuitumikia klabu ya Wekundu wa Msimbazi hao.

Abebayor ambaye hadi sasa ana mabao sita kwenye mechi za hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, alikuwa miongoni mwa wachezaji wa Gendarmerie walioshuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi wakati wakichezea kichapo cha mabao 4-0 dhidi ya Simba.

Kwa matokeo hayo, kutoka Kundi D, Simba imetinga robo fainali sambamba na RS Berkane ya Morocco huku Gendarmerie na Asec Mimosas wakiaga michuano hiyo kwa msimu huu.

Baada ya mechi hiyo wakati Gendarmerie wakiondoka uwanjani hao wakiwa ndani ya basi, mashabiki wa Simba walilizunguka na kuanza kuimba Adebayor nani? Adebayor nani? Adebayor karibu Simba...

"Nani? Adebayor, nani? Adebayor karibu Simba, wee Adebayor, Adebayor....," waliimba mashabiki wa Simba.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema kuwa atamwambia Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji 'kuvunja benki' ili kumsajili mchezaji huyo kwa ajili ya msimu ujao wa ligi na mechi za kimataifa.

Naye akizungumzia usajili hivi karibuni, Dewji alisema hivi sasa wameshakuwa na uzoefu na soka la Afrika hasa kuhusu usajili, hivyo wanapofanya kazi hiyo kwa sasa huwa hawapigi kelele, wala kusemasema kwenye vyombo vya habari.

Hatua hiyo inakuja baada ya Adebayor wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Simba nchini Niger, kueleza kuwa hakuna mchezaji ambaye asingependa kuichezea klabu kama Simba kutokana na ubora wake Afrika.



Michezo

Jumanne Aprili 5 , 2022

Nipashe



Adebayor apewa heshima Simba UKURASA 23

ROBO HIYOOO...




Mshambuliaji wa Simba, Chris Mugalu, akishangilia baada ya kuiandikia timu yake bao la tatu wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya US Gendarmerie na kutinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. Anayeshangilia nyuma ni Shomari Kapombe. **PICHA: SIMBA**

## Ajibu aitisha Yanga SC

**Na Dennis Fussi**

WAKATI kesho Azam FC ikitarajiwa kuikaribisha Yanga katika Uwanja wa Azam Complex ulioko Chamazi, Dar es Salaam, Kiungo wa timu hiyo, Ibrahim Ajibu, amewataka wageni wao hao katika mchezo ujao wa Ligu Kuu Tanzania Bara, kujiandaa kwa kipigo.



Akizungumza na gazeti hili, kiungo huyo amesema mazoezi na mbinu wanazopewa na Kocha Mkuu, Abdilhamid Moallin (pichani), ni kielelezo tosha kwanba hawapo tayari kupoteza mechi hiyo ya kesho, Jumatano.

"Tunajua kama Yanga ni timu nzuri na wanaongoza ligi, lakini tumejipanga kukabiliana nao na kuchukua pointi zote tatu," alisema Ajibu ambaye pia amewahi kuichezea Yanga na Simba kabla ya kutua Azam FC.

Yanga inaongoza msimamo wa ligi ikiwa na pointi 48 baada ya michezo 18 huku Azam ikishika nafasi ya tatu kwa alama zake 28, saba nyuma ya Simba iliyopo nafasi ya pili.

# Simba mdomoni mwa vinara CAF

## Kuivaa Al Ahly Tripoli, Orlando Pirates ama TP Mazembe, droo leo, Kocha Asec aipeleka nusu fainali...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutinga hatua ya robo fainali kwa kishindo usiku wa kuamkia jana, wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba, wameangukia mdomoni mwa vinara wa makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Simba ambayo juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa iliichapa US Gendarmerie ya Niger kwa mabao 4-0, ushindi huo umeiwezesha kumaliza nafasi ya pili kwenye Kundi D la michuano hiyo, ikiwa na pointi 10 sawa na vinara RS Berkane ya Morocco ambayo siku hiyo nayo iliichapa Asec Mimosas ya Ivory Coast bao 1-0.**

Katika makundi mengine ya michuano hiyo ya CAF, Kundi A vinara ni Al Ahly Tripoli ya Libya iliyomaliza na pointi 13 sawa na Pyramids ya Misri iliyoko nafasi ya pili, wakati Kundi B, likiongozwa na Orlando Pirates ya Afrika Kusini yenye alama 13 ikifuatiwa na Al-Ittihad ya Libya yenye pointi 11 huku Kundi C, TP Mazembe ikiongoza kwa alama zake 11, moja mbele ya Al Masry ya Misri iliyomaliza ya pili.

Droo ya hatua ya robo fainali inatarajiwa kuchezeshwa leo Makao Makuu ya CAF jijini Cairo, Misri kabla ya mechi za hatua hiyo kupigwa Aprili 17, mwaka huu kwa mtindo wa nyumbani na ugenini.

Kwa mujibu wa kanuni za mashindano hayo upangaji wa droo utazingatia timu zilizotoka kundi moja hazitakutana katika robo fainali, lakini mshindi wa kwanza katika kila kundi atakutana na mshindi wa pili kutoka kundi lingine.

Hivyo, Simba ambayo imeshika nafasi ya pili kutoka Kundi D, katika droo hiyo ya leo, uwezekano uliopo ni kukutana na Al Ahly Tripoli, Orlando Pirates ama TP Mazembe ambazo ni vinara wa Kundi A, B na C, wakati RS Berkane kinara wa Kundi D, yenyewe inaweza kuangukia mdomoni mwa Pyramids, Al-Ittihad au Al Masry zilizoshika nafasi ya pili kutoka Kundi A, B na C.

Kuelekea droo hiyo leo, baada ya ushindi wa jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana mwanzo mwisho licha ya kupoteza nafasi nyingi kipindi cha kwanza, lakini akawapongeza mashabiki kwa kujitoa usiku kwenda kuishangilia timu yao.

Hata hivyo, Pablo alisema hatua inayofuata ya robo fainali itakuwa ngumu zaidi kwa kuwa watakutana na timu bora zilizomaliza nafasi ya kwanza katika makundi yao, hivyo wataenda kujipanga kukabiliana na ushindani watakaokutana nao.

"Niwapongeza wachezaji wangu kwa namna walivyojitoa na kujituma, pamoja na mashabiki waliojitokeza kwa wingi uwanjani usiku wa leo [juzi] kuisapoti timu licha ya mchezo kuanza katika muda ambao haukuzoeleka.

"Tunakwenda sasa kukutana na timu bora zilizoongoza makundi zenye uzoefu mkubwa, tunatambua itakuwa mechi ngumu zaidi, lakini Simba pia ni timu kubwa tutajipanga," alisema.

Hata hivyo, baada ya kikosi chake kumaliza nafasi ya tatu kikiwa na pointi tisa, Kocha Mkuu wa Asec Mimosas, Julien Chevalier, amesema Kundi lao la D, ndilo lilikuwa na timu bora zaidi, hivyo kutokufuzu kwao hakuna maana kwamba walizembea.

Akizungumza baada ya mechi yao dhidi ya Berkane kumalizika juzi nchini Morocco, Chevalier alisema timu zilizopita katika Kundi D, huenda bingwa akatokea hapo iwe Simba ama Berkane kutokana na ubora wao.

Kwa kutinga robo fainali, timu zote zilizoingia hatua hiyo, kila moja italamba Dola za Kimarekani 350,000 sawa na Sh. milioni 809.6 za Tanzania huku zilizoishia hatua ya makundi kwa kushika nafasi ya tatu na nne katika kila kundi, kila moja ikiondoka na Sh. milioni 632.

Timu zitakazofuzu nusu fainali zitaondoka na Sh. bilioni moja, wakati bingwa wa michuano hiyo akiondoka na Sh. bilioni 2.8 na mshindi wa pili Sh. bilioni 1.4.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >